



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2008/09

Wizara ya Fedha na Uchumi
S. L. P 9111
Dar es Salaam
TANZANIA

Juni, 2008

YALIYOMO

UTANGULIZI	ii
SURA YA KWANZA	1
HALI YA UCHUMI WA TAIFA.....	1
1.1 Pato la Taifa.....	1
1.6 Ujazi wa Fedha	3
1.7 Mwenendo wa Riba na Mikopo ya Benki za Biashara	3
1.8 Thamani ya Shilingi.....	4
1.9 Deni la Taifa.....	4
SURA YA PILI.....	6
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI - 2007/08.....	6
Eneo la Kwanza: Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato.....	6
Eneo la Pili: Uboreshaji wa Hali ya Maisha na Maendeleo ya Jamii	24
Eneo la Tatu: Utawala Bora na Uwajibikaji	29
SURA YA TATU	39
Utekelezaji wa MKUKUTA katika mwaka 2008/09	41
Eneo la Kwanza: Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato.....	41
Eneo la Pili: Uboreshaji wa Hali ya Maisha na Maendeleo ya Jamii	56
Eneo la Tatu: Utawala Bora na Uwajibikaji	61
SURA YA NNE	72
PROGRAMU ZA WIZARA NA TAASISI MBALIMBALI.....	72
PROGRAMU ZA MIKOA	97
SURA YA SITA	132
MFUMO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MIRADI YA MAENDELEO	132

UTANGULIZI

1. Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya 2008/09-2010/11 unasisitiza utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika Mwongozo wa bajeti ya 2008/09. Mwongozo huo unaelekeza utaratibu wa kuzingatia vipaumbele katika kuandaa na kutekeleza programu na miradi ili kuleta msukumo wa haraka katika maendeleo ya uchumi wa Taifa. Aidha, Mpango huu unaendelea kusisitiza umuhimu wa kumaliza miradi inayoendelea ili kupata matokeo katika kipindi kifupi.
2. Dira ya Maendeleo 2025 yenye upeo wa muda mrefu inabainisha malengo ya maendeleo ya muda mrefu, mwelekeo na vipaumbele vitakavyotekelezwa ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kiuchumi, kijamii na kiteknolojia. Utekelezaji wa Dira ambao ni wa vipindi vya muda wa kati wa miaka mitatu mitatu umeendelea kuboreshwa kwa kusisitiza kuwa na vipaumbele na miradi michache inayoweza kukamilika katika muda mfupi na kuleta matokeo ya haraka katika jamii.
3. Mambo mengine ya kuzingatia katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2008/09 kama yalivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Mpango na Bajeti ni pamoja na yafuatayo:-
 - i. Mikoa na sekta zote ziendee kubaini na kuendeleza fursa za maendeleo zinazovutia uwekezaji wa sekta binafsi pamoja na kuwahamasisha wananchi wawekeze kwa lengo la kuchochea maendeleo yao;
 - ii. Sheria na kanuni zinazosimamia mashirika na taasisi za umma zinazokusanya maduhuli zitaendelea kuhuishwa ili sehemu kubwa zaidi ya makusanyo hayo iweze kuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kuchangia katika maendeleo ya Taifa;

- iii. Taratibu za kufuatilia utekelezaji wa mpango na bajeti (Monitoring of Plan and Budget Execution) zitaendelea kuimarishwa.
4. Kiasi cha rasilimali kilichokadiriwa kwa mpango mzima wa mwaka 2008/09 ni sh. 2, 489,480 milioni. Kati ya hizo, fedha za ndani ni sh. 938,380 milioni sawa na asilimia 38 na fedha za nje ni sh. 1, 551,100 milioni sawa na asilimia 62. Aidha, sh. 2, 099,786.6 milioni sawa na asilimia 84 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza programu zinazosimamiwa na wizara na idara za serikali na sh. 389,693.4 milioni sawa na asilimia 16 ya bajeti yote ya miradi ya maendeleo zitatumika kutekeleza programu zitakazosimamiwa na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

SURA YA KWANZA
HALI YA UCHUMI WA TAIFA

1.1 Pato la Taifa

Mwenendo wa hali ya uchumi katika mwaka 2007 umeendelea kuwa mzuri licha ya nchi kukabiliwa na ukame pamoja na matatizo ya umeme yaliyoikumba nchi katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. Mwenendo mzuri wa uchumi jumla ni matokeo ya mageuzi katika sekta za kiuchumi na kijamii yaliyoanza tangu mwaka 1992. Matokeo ya mageuzi hayo yamepelekea kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji uchumi (GDP) katika miaka ya hivi karibuni kwa wastani wa kiwango cha asilimia 7.0 kwa mwaka tangu mwaka 2001. Kiwango hiki ni cha juu zaidi ya wastani wa ukuaji wa uchumi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Pato halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 7.1 katika mwaka 2007 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2006.

1.2 Kasi ya Upandaji Bei

Wastani wa kasi ya upandaji bei ulikuwa asilimia 7.0 mwaka 2007 ikilinganishwa na asilimia 7.3 mwaka 2006. Hata hivyo, matatizo ya ukame na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia yalisababisha kuendelea kuongezeka kwa kasi ya upandaji bei. Hadi kufikia mwezi Aprili 2008, kasi ya upandaji bei ilikuwa asilimia 9.7, baada ya kupanda kutoka asilimia 9.0 mwezi wa Machi, 2008. Kiwango hicho kinatarajiwa kushuka, kutokana na ongezeko la upatikanaji wa chakula baada ya kipindi cha mavuno kuanza katika sehemu nyingi za nchi.

1.3 Ukuzaji Rasilimali

Katika mwaka 2007, ukuzaji rasilimali uliongezeka na kufikia sh. 6,209,741 milioni kutoka sh. 4,957,781 milioni mwaka 2006, kwa bei za mwaka husika, sawa na ongezeko la asilimia 25.3. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 29.6 kwa bei za mwaka husika ikilinganishwa na asilimia 27.6 mwaka 2006. Kuongezeka kwa

ukuzaji rasilimali kulitokana hasa na ongezeko katika ujenzi wa majengo; uagizaji wa vifaa vya uwekezaji mitaji; na kuongezeka kwa shughuli nyinginezo za ukuzaji rasilimali zikiwemo uendelezaji ardhi, barabara na madaraja

1.4 Mapato na Matumizi

Mapato yatokanayo na kodi yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka hasa kutokana na kuimarika kwa makusanyo ya kodi na yale yasiyo ya kodi. Wastani wa makusanyo ya kodi kwa sasa umefikia sh. 293.2 bilioni kwa mwezi ikilinganishwa na sh. 25 billioni zilizokuwa zinakusanya kwa mwezi katika kipindi cha miaka ya tisini (Mid 1990s). Kwa upande mwingine, matumizi ya serikali yamekuwa yakiongezeka hasa katika sekta za uzalishaji na juhudi za kupunguza umaskini nchini. Fedha nyingi zimekuwa zikielekezwa katika uboreshaji wa utumishi wa umma na kuendeleza mageuzi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ikiwamo utekelezaji wa MKUKUTA.

1.5 Biashara Nje

Mauzo ya bidhaa nje yameanza kuimarika hasa mauzo ya bidhaa zisizo asilia kama samaki na dhahabu. Sekta ndogo ya utalii inakua kwa haraka kutokana na juhudi za Serikali za kuutangaza utalii na vivutio vya utalii ndani ya nchi na katika vituo mbalimbali duniani. Uagizaji wa bidhaa nje umeongezeka kwa kiasi hasa uagizaji wa bidhaa za uwekezaji mitaji na zile za kati kama mafuta kwa ajili ya kuendesha mitambo mbalimbali viwandani, wakati ambapo uagizaji wa bidhaa za walaji umeanza kupungua. Aidha, hadi kufikia Disemba 2007, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 4.9.

1.6 Ujazi wa Fedha

Katika mwaka ulioishia Desemba 2007, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M_2)¹ uliongezeka kwa asilimia 28.8 ikilinganishwa na asilimia 13.7 Desemba 2006. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M_3) ulikuwa asilimia 21.4 Desemba 2007, ikilinganishwa na asilimia 22.0 Desemba 2006. Ongezeko la M_2 lichangiwa na kuongezeka kwa amana za hundi kulikotokana na kuboreka kwa viwango vya riba. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi ulikuwa unakua kwa kiwango kidogo kutokana kuimarika kwa thamani ya shilingi kulikosabisha amana za fedha za kigeni kuongezeka kwa kiwango kidogo.

1.7 Mwenendo wa Riba na Mikopo ya Benki za Biashara

Mikopo kwa sekta binafsi iliendeleo kuongezeka katika mwaka 2007. Hadi kufikia mwezi Disemba mwaka 2007, mikopo iliyoelekezwa katika sekta binafsi ilifikia asilimia 42.2 zaidi ya lengo lililowekwa la asilimia 34.8. Mikopo katika sekta hii iliongezeka kutoka sh.2,028,294.3 milioni Disemba 2006 hadi sh. 2,883,789.5 milioni Disemba 2007. Mikopo mingi ilielekezwa katika shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani (asilimia 19.3); biashara (asilimia 17.2); kilimo (asilimia 9.9); usafirishaji na mawasiliano (asilimia 7.0).

Wastani wa riba zilizotozwa na benki mbalimbali za biashara umeendelea kuwa na tofauti kubwa kati ya riba za amana na zile za kukopa. Wastani wa riba za mikopo katika benki za biashara uliongezeka kutoka asilimia 15.66 mwaka 2006 hadi asilimia 16.03 mwaka 2007. Aidha, riba za amana na uwekaji akiba zilipungua kutoka asilimia 2.61 mwaka 2006 hadi asilimia 2.59 mwaka 2007. Ongezeko la wastani wa riba za mikopo na amana ilinaashiria kuwa bado tofauti kati ya riba za mikopo na amana inazidi kuongezeka katika uchumi.

¹ M_0 ni fedha zilizo kwenye mzunguko nje ya mabanki; $M_1 = M_0 +$ amana za hundi; $M_2 = M_1 +$ amana za muda maalum + amana za akiba;
 $M_3 = M_2 +$ amana za fedha za kigeni (foreign deposits)

1.8 Thamani ya Shilingi

Thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani kwa mwaka 2007, ilikuwa na wastani wa sh. 1,2791.1 kwa dola moja, ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,251.9 kwa dola moja mwaka 2006. Mwenendo huo ni sawa na kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kwa asilimia 2.2. Aidha, thamani ya shilingi kwa dola moja ilikuwa sh. 1,132.1 mwishoni mwa Disemba 2007 ikilinganishwa na sh. 1,261.6 mwishoni mwa Disemba 2006. Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani kulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kugharamia uagizaji wa bidhaa toka nje, hususan mafuta, na kushuka kwa dola ya kimarekani ikilinganishwa na sarafu nyinginezo.

1.9 Deni la Taifa

Hadi Disemba 2007, deni la Taifa lilifikia dola za Marekani 7,041.3 milioni ikilinganishwa na dola za Marekani 7,188.4 milioni Desemba 2006, ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 2.0. Kupungua kwa deni la Taifa kulitokana hasa na juhudi za serikali za kuhakikisha kuwa madeni yamelipwa kwa wakati na kuendelea kupatiwa misamaha na nchi wahisani wanachama wa Paris Club na washirika wengine wa maendeleo. Vilevile, kuyumba kwa thamani ya dola ya Marekani ikilinganishwa na sarafu nyingine katika soko la fedha pia kulichangia kupungua huko. Hadi kufikia Disemba mwaka 2007, deni la nje lilikuwa jumla ya Dola za kimarekani 5,367.7 milioni na lile la ndani dola 1,673.5 milioni, sawa na asilimia 76.2 na 23.8 ya deni lote kwa mtiririko huo.

Hadi kufikia mwezi Disemba mwaka 2007, serikali ililipa madeni yake yenye thamani ya dola za marekani 46.1 milioni. Kati ya fedha hizo dola 27.2 milioni zililipia mkopo halisi na dola 18.9 milioni zilikuwa malipo ya riba. Msamaha wa madeni kutokana na mpango wa kuzifutia madeni nchi maskini zaidi dunia (HIPIC) na Msamaha wa madeni

kutoka mashirika ya kimataifa ndio vilivyochangia kwa kiasi kikubwa katika ulipaji wa madeni nchini.

Hadi kufikia Disemba mwaka 2007, deni la ndani lilikuwa shilingi 1,894.6 bilioni. Sehemu kubwa ya deni la ndani ilitokana na uuzaji wa hawala za serikali, ambapo hawala hizo zilichukua asilimia 99.6 ya deni lote la ndani.

SURA YA PILI
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA
KUPUNGUZA UMASKINI - 2007/08

2.1 Utangulizi

Hatua mbalimbali za kukuza uchumi na kupunguza umaskini zilichukuliwa katika mwaka 2007/08. Katika eneo la kwanza la MKUKUTA, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuendeleza mageuzi ya kiuchumi na mageuzi katika sekta ya fedha (Financial Sector Reforms), kuvutia uwekezaji, kuongeza ajira, kuongeza mauzo nje ya nchi, kujenga na kuboresha miundombinu, kuendeleza rasilimali watu, na kupanua kilimo cha umwagiliaji.

Aidha, hatua zilizochukuliwa katika eneo la pili la MKUKUTA ni pamoja na kutekeleza programu mbalimbali katika sekta za elimu, afya, Maji na ustawi wa jamii. Katika eneo la utawala bora na uwajibikaji, serikali ilielekeza nguvu katika kupiga vita rushwa, kuboresha ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinagawiwa kwa usawa. Aidha serikali ilitoa kipaumbele katika kuimarisha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pamoja na sheria na taratibu za manunuzi.

Eneo la Kwanza: Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato

2.2 Sekta Ya Kilimo

2.2.1 Utangulizi

Katika kufikia malengo ya MKUKUTA na Dira ya Maendeleo 2025, Serikali kwa mwaka 2007/08 iliendelea kutekeleza mipango na programu ambazo zililenga katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini ili kuwavutia wawekezaji wengi katika sekta ya kilimo. Aidha, maeneo mengine yaliyopewa kipaumbele katika utekelezaji ni kupanua kilimo cha umwagiliaji; kuhakikisha upatikanaji wa mbolea na madawa ya kuulia wadudu na kuboresha huduma za ugani.

2.2.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika mwaka 2007/08, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika sekta ya kilimo ni kama yafuatayo:-

- i. Kuendelea kushiriki katika kuandaa mkakati wa matumizi bora ya ardhi;
- ii. Kuimarisha mikakati ya kuwavutia wawekezaji binafsi katika sekta ya kilimo;
- iii. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa kupanua na kuhimiza kilimo cha umwagiliaji;
- iv. Kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya matumizi ya vifaa mbalimbali vya umwagiliaji ; na
- v. Kuviwezesha vyama vya wazalishaji kuzalisha mazao ambayo yanakidhi matakwa ya soko la ndani na nje.

b) Utekelezaji

Utekelezaji wakatika maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika sekta ya kilimo, kwa mwaka 2007/2008, ulikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Sekretariat za Mikoa zilijengewa uwezo wa kusaidia Halmashauri za wilaya kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Wilaya (DADPs);
- ii. Idadi ya vyuo vinavyotoa mafunzo ya kilimo iliongezeka kutoka vyuo 7 hadi vyuo 11;
- iii. Kupanua kilimo cha umwagiliaji kutoka hekta 264,388 hadi hekta 283,133;
- iv. Upembuzi yakinifu katika mabwawa 4 na skimu 31 zitakazowezesha hekta 51,568 kuendelezwa chini ya umwagiliaji umefanyika.

2.3 Mifugo

2.3.1 Utangulizi

Sekta ndogo ya mifugo ni nguzo mojawapo muhimu katika kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya jamii. Mchango wa sekta hii unajumuisha kuongeza upatikanaji wa chakula na lishe, nguvu kazi wanyama, biashara, mbolea ya samadi kwa kilimo endelevu na nishati.

2.3.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika mwaka 2007/08 maeneo yaliyopewa kipaumbele ili kufanikisha malengo ya sekta ya mifugo yalikuwa kama yafuatayo:-

- i. Kujenga na kuimarisha miundombinu mbalimbali ya mifugo kama vile majosho na malambo;
- ii. Kuimarisha uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine wanaotoa huduma za mifugo;
- iii. Kuboresha mifumo ya malisho, tija, usindikaji na masoko ya bidhaa za mifugo;
- iv. Kuongeza upatikanaji wa pembejeo bora za mifugo, mazao ya mifugo na huduma za ukaguzi; na
- v. Kuandaa na kutekeleza mpango wa kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya mifugo.

b) Utekelezaji

Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2007/2008, ulikuwa kama ifuatayo:

- i. Kanuni na miongozo inayohusu Sekta ya Mifugo imeendelea kuhuishwa na mapendekezo ya kurekebisha sheria mbalimbali yameandaliwa;
- ii. Kwa kushirikiana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yakiwemo ya Heifer Project Tanzania (HPT) na Southern Highlands Livestock Development Association (SHILDA) jumla ya mitamba 6,721 imesambazwa kwa wananchi;

- iii. Miundombinu ya masoko ya mifugo ya Lumecha (Songea), Buhigwe (Kasulu), Kasesya (Sumbawanga) na Mbuyuni (Chunya) imeendelea kuboreshwa; na
- iv. Tani 26 za Mbegu bora za malisho na marobota 306,000 ya hei yalizalishwa na kuuzwa na Taasisi za Serikali na sekta binafsi.

2.4 Ushirika na Masoko

2.4.1 Utangulizi

Eneo la ushirika na masoko lilipewa msukumo wa pekee katika kuboresha njia mbali mbali za kuinua kipato cha wananchi walio wengi hususan waishio vijijini. Katika mwaka 2007/08 msisitizo ulikuwa katika uzalishaji wa mazao na kuongeza nguvu ya umiliki wa soko.

2.4.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika mwaka 2007/08 maeneo ya kipaumbele yalikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Kuboresha upatikanaji wa mikopo ya uendelezaji wa ushirika na masoko katika ngazi zote;
- ii. Kuimarisha shughuli za ushirika na masoko ili kuongeza pato la wananchi;
- iii. Kuongeza upatikanaji wa masoko kwa mazao ya chakula na ya biashara na kuyatumia kikamilifu; na
- iv. Kuongeza ubora wa bidhaa ili kuweza kukabiliana na ushindani katika soko la ndani na nje.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08 utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Mafunzo ya usimamizi, biashara na stadi za ujasiriamali yalitolewa kwa wajumbe wa bodi za vyama vya ushirika Kahama, Tabora, Chunya, Rukwa, Songea na Manyoni;

- ii. Wahasibu 35 wa SACCOS walipewa udhamini wa kozi ya miezi 9 katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara (MUCCoBS). Wahasibu hao walitoka katika mikoa ya Shinyanga (10), Mtwara (6), Kilimanjaro (1), Pwani (2), Manyara (8) na Dodoma (8);
- iii. Zoezi la kuainisha Vyama vya Ushirika wa akiba na Mikopo katika madaraja liliendelea;
- iv. Miongozo na maelekezo ya kuboresha utendaji katika Shirikisho la Vyama Vya Ushirika (TFC) na Chama Kikuu cha Vyama vya Akiba na Mikopo (SCCULT) iliandaliwa.

2.5 Barabara

2.5.1 Utangulizi

Sekta ndogo ya barabara ina umuhimu wa pekee katika kufanikisha shughuli za Sekta nyingine za kiuchumi na kijamii nchini hususan kilimo, mifugo, utalii na uzalishaji viwandani.

2.5.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

- a) Maeneo ya kipaumbele
Maeneo ya kipaumbele katika sekta ndogo ya barabara yalikuwa kama ifuatavyo:-
 - i. Kutekeleza Programu ya Uwekezaji katika Miundombinu ya Uchukuzi (TSIP);
 - ii. Kujenga jumla ya kilomita 527.5 za barabara kwa kiwango cha lami. Kati ya hizo, kilomita 470.5 ni Barabara Kuu na kilomita 57 ni Barabara za Mikoa;
 - iii. Kuratibu usalama na utunzaji wa mazingira katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu; na
 - iv. Kuainisha maeneo ya kufanya utafiti.

b) Utekelezaji

Mwaka 2007/08 utekelezaji katika sekta ndogo ya barabara ulikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Katika kundi la barabara kuu, kilomita 318 zilijengwa kwa kiwango cha lami wakati kilomita 78 za lami na 153 za changarawe zilikarabatiwa; na kilomita 5,080.4 za lami zilifanyiwa matengenezo;
- ii. Katika kundi la barabara za Mikoa, kilomita 365 za changarawe na 15 za lami zilikarabatiwa, wakati kilomita 4,172.7 za barabara za lami na 4,295.5 za barabara za changarawe zilifanyiwa matengenezo;
- iii. Jumla ya kilomita 3,181 za barabara za halmashauri zilikarabatiwa;
- iv. Jumla ya madaraja 32 ya barabara kuu na madaraja 42 ya barabara za mikoa yalifanyiwa matengenezo; na
- v. Maandalizi ya utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Uchukuzi (The Transport Sector Investment Program-TSIP) ambao unalenga kuhakikisha kuwa mpaka mwaka 2018 barabara kuu zote ziwe katika kiwango cha lami ulikamilishwa.

2.6 Mawasiliano na Uchukuzi

2.6.1 Utangulizi

Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika utoaji wa fedha na kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa njia kuu za mawasiliano zikiwemo: reli, simu, posta, bandari na barabara.

2.6.2 Mapitio ya Mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Mwaka 2007/08, sekta ya mawasiliano na uchukuzi iliendelea kutekeleza maeneo ya kipaumbele yafuatayo:-

- i. Kusimamia, kudhibiti, kutoa elimu, kuhamasisha katika kutoa huduma bora za mawasiliano nchini ikiwemo mipango ya kuboresha na kupanua njia kuu za mawasiliano (Digital Microwave Backbone), mpango wa kuanzisha vituo vipya vya “Tele Centre” na kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya habari;
- ii. Kujenga na kukarabati miundombinu ya viwanja vya ndege, bandari, magati, reli na mtandao wa mawasiliano;
- iii. Kuoanisha viwango vya usafirishaji na mawasiliano vya ndani na vya kimataifa; na
- iv. Kuratibu vyombo vya usafiri wa abiria ili kupunguza ajali.

b) Utekelezaji

Utekelezaji wa malengo ya sekta ya mawasiliano na uchukuzi kwa mwaka 2007/08 ilikuwa kama ifuatavyo

- i. Mamlaka ya Bandari nchini iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kuendeleza bandari ikiwemo uwekezaji katika mitambo ya kupakua na kushusha mizigo na kuendeleza miundombinu iliyopo;
- ii. Serikali iliingia ubia na wawekezaji kutoka India katika kuendesha Shirika la Reli (TRC) na kuundwa kwa Kampuni ya Reli Nchini (TRL) inayotoa huduma hizo. TRL imefanikiwa kurejesha huduma za uchukuzi kwa njia ya reli kati ya Dar es salaam na Dodoma;
- iii. Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Mkonga wa kitafa wa mawasiliano umekamilika;
- iv. Ukarabati wa Viwanja vya ndege vya Mwanza, Singida, Mafia na Arusha, na ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe uliendelea; na
- v. Upembuzi yakinifu kwa ajili ya ununuzi wa kivuko cha Kigamboni umefanyika na uunganishaji wa kivuko hicho umeanza.

2.7 Sekta ya Ardhi

2.7.1 Utangulizi

Katika mwaka 2007/08, serikali ililenga kutoa huduma za upimaji wa ardhi katika maeneo mapya na kutoa leseni za makazi kwa maeneo yaliyojengwa kiholela katika mkoa wa Dar es Salaam. Pia iliendelea na programu ya kupima mipaka ya vijiji, miji, mikoa na kutoa hati za kimila za kumiliki ardhi katika baadhi ya vijiji hapa nchini.

2.7.2 Mapitio ya Mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika mwaka 2007/08, maeneo ya kipaumbele ya sekta ya ardhi yalikuwa yafuatayo:-

- i. Kuendeleza huduma za upimaji wa viwanja na ramani;
- ii. Kuandaa mazingira mazuri ya makazi ya gharama nafuu na endelevu;
- iii. Kuendeleza mpango wa kusimamia ukuaji na uendelezaji wa miji;
- iv. Kuwamilikisha wananchi wa mijini na vijijini maeneo yaliyopimwa;
- v. Kuweka mipaka rasmi ya vijiji, miji, mikoa na taifa;
- vi. Kuwa na kumbukumbu sahihi za ardhi na zinazopatikana kwa urahisi kwenye tarakishi;
- vii. Kutoa elimu juu ya sera na sheria ya ardhi na
- viii. Kupunguza kasi ya ujenzi katika maeneo yasiopimwa na yenye upungufu wa utoaji wa huduma muhimu za jamii.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/2008, sekta ya ardhi ilitekeleza yafuatayo:-

- i. Vijiji 211 vilipata vyeti vya Ardhi na wananchi wapatao 3,940 walipata hati za kimila;

- ii. Hati za kumiliki Ardhi zipatazo 7, 778 zilisajiliwa na maombi 7,468 ya upekuzi katika daftari la hati (Official Search) yalipokelewa na kushughulikiwa;
- iii. Mashauri 6,141 kati ya mashauri yote 13,074 kwa mwaka 2007 yaliamuliwa, na mashauri mengine 6,933 yalibakia yakiendelea kusikilizwa. Aidha, Mabaraza 10 ya Ardhi na Nyumba katika Wilaya za Njombe, Rungwe, Mbinga, Simanjiro, Same, Karatu, Chato, Geita, Tarime na kilombero yaliundwa;
- iv. Jumla ya Viwanja 20,173 na mashamba 706 yalipimwa nchini kote. Aidha, hadi Desemba 2007 Vijiji 3204 vilikuwa vimepimwa mipaka yake;
- v. Jumla ya Ramani za awali 8 za Miji ya Tarime, Magu, Shirati, Kisesa, Misasi, Sirari, Kamachumu na Ngara katika Kanda ya Ziwa zilitayarishwa na kukamilika. Maandalizi pia yalianza kwa Miji mingine 28;
- vi. Jumla ya taarifa za Viwanja 52,750 kati ya Viwanja 109,500 kutoka Ofisi za Ardhi za Halmashauri za Tanga, Musoma, Shinyanga, Kahama, Tabora, Kibaha, Mtwara na Iringa zilitambuliwa na kuingizwa kwenye tarakishi kwa lengo la kuboresha makusanyo ya kodi ya pango la ardhi katika Wilaya husika;
- vii. Leseni za Makazi 16,589 zilitolewa na maombi 9,442 yalipokelewa. Wamiliki 150 walitumia Leseni za makazi kupata mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha. Aidha, wamiliki 23,000 walitambuliwa na taarifa zao kuingizwa kwenye hazina ya kumbukumbu.

2.8 Sekta ya Nishati

2.8.1 Utangulizi

Katika mwaka 2007/08 Serikali ililenga kutimiza azma ya kuwa na nishati nafuu na ya uhakika na kupanua wigo wa vyanzo vya nishati.

2.8.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika mwaka 2007/08 sekta ya nishati ililenga kutekeleza maeneo ya kipaumbele yafuatayo:-

- i. Kusambaza umeme katika Wilaya za Bukombe, Kilolo, Ludewa, Kilindi, Mbinga na Simanjiro;
- ii. Kuimarisha njia kubwa za umeme, na kuboresha usambazaji katika vituo vidogo;
- iii. Kusimamia utekelezaji wa miradi ya Mnazi Bay na Songo Songo;
- iv. Kuandaa mkakati maalum wa hifadhi ya bidhaa za petroli na biashara ya petroli; na
- v. Kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08, sekta ya nishati ilitekeleza yafuatayo:-

- i. Kukamilisha uanzishwaji wa Wakala na Mfuko wa nishati Vijijini - Rural Energy Agency [REA] ambao utawezesha upelekaji wa nishati ya kisasa Vijijini;
- ii. Wateja katika Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma waliendelea kuunganishwa kwenye mfumo wa umeme baada ya kukarabatiwa jenereta yenye uwezo wa kuzalisha kVA 320 mwezi Septemba, 2006;
- iii. Serikali iliingia mkataba na mkandarasi wa kutengeneza, kusimika jenereta mbili zenye uwezo wa kuzalisha kVA 1,250 kila moja kwa ajili ya wilaya ya Mbinga na jenereta nyingine mbili zenye uwezo wa kuzalisha kVA 600 kila moja kwa ajili ya wilaya ya Ludewa;
- iv. Ujenzi wa Mtambo unaotumia gesi asilia unaomilikiwa na TANESCO wenye uwezo wa kuzalisha MW 100 ulikamilika; na
- v. Rasimu ya Mkataba wa uendeshaji wa Mradi wa Gesi ya Mnazi bay kati ya Serikali na Kampuni ya Artumas iliandaliwa.

2.9 Sekta ya Madini

2.9.1 Utangulizi

Mwaka 2007/08 Serikali pamoja na mambo mengine, ilizingatia kujenga uwezo wa wachimbaji wadogo na wa kati kwa kuwapatia teknolojia iliyo bora na kuongeza thamani ya madini kabla ya kuyauza na kuhakikisha kuwa wale walio jirani na migodi pamoja na taifa wanafaidika.

2.9.2 Mapitio ya Mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Mwaka 2007/08 maeneo ya kipaumbele katika Sekta ya Madini yalikuwa yafuatayo:-

- i. Kuhamasisha maendeleo ya uwekezaji katika sekta ya madini;
- ii. Kuongeza thamani ya madini;
- iii. Kuweka mikakati itakayoboresha na kuendeleza wachimbaji wadogo na wa kati;
- iv. Ujenzi wa maghala ya kuhifadhi udongo wa madini (cores from exploration) kwa ajili ya makampuni ya madini;

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08, sekta ya madini ilitekeleza yafuatayo:-

- i. Sera ya Madini ya mwaka 1997 na sheria ya madini ya mwaka 1998 iliendelea kufanyiwa marekebisho; hii ikiwa ni pamoja na kupitia upya mikataba ya madini;
- ii. Mfumo mpana wa kumbukumbu za utafutaji na uchimbaji madini unaounganisha ofisi 21 za madini na makao makuu ulianza kufanya kazi;
- iii. Maabara ya kutathmini kiwango (concentrate) cha sampuli za dhahabu kutoka kwa wachimbaji wakubwa wa dhahabu ilifunguliwa rasmi;

- iv. Ofisi ya madini mkoani Kigoma ilifunguliwa kwa lengo la kusimamia na kurahisisha shughuli za wachimbaji madini wadogo na wakubwa; na
- v. Kuendelea kufanya majadiliano na makampuni ya madini kwa lengo la kuhakikisha wadau wanafaidika.

2.10 Maliasili na Utalii

2.10.1 Utangulizi

Katika mwaka 2007/08, Serikali ililenga katika kuhifadhi, kuendeleza utalii na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili na malikale iliyopo kwa ajili ya manufaa ya Taifa kwa ujumla.

2.10.2 Mapitio ya Mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika kipindi cha mwaka 2007/08, shughuli za kipaumbele zilizopangwa kutekelezwa zilikuwa ni pamoja na:-

- i. Kuboresha mazingira yatakayoweza wadau kushiriki kikamilifu katika uhifadhi wa maliasili, malikale na vivutio vya utalii;
- ii. Kuimarisha ukusanyaji maduhuli ya Serikali;
- iii. Kudhibiti uvunaji haramu na uvunjaji wa sheria zinazosimamia maliasili, malikale na utalii; na
- iv. Kupitia Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia maliasili, malikale na utalii.

b) Utekelezaji

Utekelezaji katika Sekta ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2007/08 ni kama ifuatavyo:-

- i. Mapitio ya sera na sheria za misitu, ufugaji nyuki na utalii yalifanyika; Sera mpya ya wanyamapori ya mwaka 2007 ilikamilika na kupitishwa rasmi;

- ii. Mpango Mkakati wa Kitaifa wa kusimamia Ardhievu ulitayarishwa na utekelezaji wake umeanza mara baada ya kupitishwa Sera mpya ya Wanyamapori;
- iii. Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Sura ya 283 ya mwaka 2000; ilifanyiwa marekebisho.
- iv. Kukamilisha mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya Malikale;
- v. Kukamilishwa na kupitishwa kwa Sheria mpya ya Utalii, na kukamilisha maandalizi ya hatua ya tatu ya Programu ya Taifa ya kuendeleza Utalii;
- vi. Kuchukua hatua za kuongeza maduhuli ambazo zilijumuisha kuimarishwa kwa kikosi cha doria cha misitu, Kuongezwa kwa viwango vya tozo na ada kwenye mazao ya misitu na nyuki na kuongezeka kwa mavuno ya miti ambayo iliuzwa kwa mnada;
- vii. Kanuni za Utalii wa Picha zimekamilika na zitatumika kuanzia mwezi Julai 2008;
- viii. Rasimu ya Mpango wa Uendelezaji na Usimamizi kwa Mapori ya Akiba ya Maswa na Ikorongo- Grumeti ilitayarishwa;
- ix. kusimamia hekta 85,000 na kurudishia miti hekta 4,237 katika mashamba 16 ya Serikali na kupanda miti maeneo mengine mapya hekta 1,107;
- x. Tathmini ya hali halisi ya ufugaji nyuki ilifanyika sambamba na kueneza Mradi wa Uboreshaji ufugaji nyuki Tanzania katika wilaya 30 nchini;
- xi. Barabara zenye urefu wa Kilomita 300 zilitengenezwa, na viwanja 8 vya ndege vilikarabatiwa na kutengenezwa katika mapori ya akiba;
- xii. Mipaka ya Pori la Mpanga-Kipengele (Kilomita 50) na Pori la Akiba la Burigi/Biharamulo (Kilomita 35) ilihakikiwa kwa pamoja na wananchi na kuwekewa alama za kudumu; na
- xiii. Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa kuhifadhi misitu ya asili na mikoko ulitekelezwa katika wilaya 24 zenye misitu ya lindimaji na wilaya 10 zenye mikoko katika ukanda wa pwani.

2.11 Sekta ya Viwanda na Biashara

2.11.1 Utangulizi

Katika mwaka 2007/08 Serikali ililenga kutekeleza shughuli zenye kuzingatia kuongeza uzalishaji wa bidhaa za kuuza nchi za nje.

2.11.2 Mapitio ya Mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika mwaka maeneo ya kipaumbele katika sekta ya Viwanda na Biashara ni pamoja na :-

- i. Kuimarisha maendeleo ya Viwanda Vidogo na vya Kati na kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwa kusindika bidhaa za kilimo;
- ii. Kuvutia uwekezaji katika uzalishaji, kuongeza upatikanaji wa soko na kuboresha teknolojia za "biogas" na mionzi ya jua;
- iii. Kuimarisha taasisi zinazojihusisha na utafiti na maendeleo;
- iv. Kutoa mafunzo ya ujasiriamali; na
- v. Kuendelea kutekeleza programu ya MKUMBITA na Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003.

b) Utekelezaji

Utekelezaji katika Sekta ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2007/08 ni kama ifuatavyo:-

- i. Mfumo wa kutoa taarifa kutoka masoko 75 hadi 93;
- ii. Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda Endelevu ulifanyiwa mapitio kwa kushirikisha sekta binafsi;
- iii. Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa wajasiriamali kupitia SIDO na vyama visivyo vya kiserikali;
- iv. Ujenzi wa Maeneo Maalumu ya Uuzaji Bidhaa Nje uliendelea; na
- v. Kuendelea kuweka mazingira bora ya biashara, kuboresha miundombinu, kuimarisha huduma za kifedha na zisizo za

kifedha na taasisi zinazochangia katika maendeleo ya Viwanda Vidogo na vya Kati.

2.12 Biashara Ndogo na za Kati (SMEs)

2.12.1 Utangulizi

Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (2003) sambamba na sera nyingine zilizolenga biashara ndogo na za kati, kama vile Sera ya Taifa ya Uwezesaji (2004); kwa lengo la kuanzisha, kuendeleza na kuimarisha ushindani wa biashara ndogo na za kati.

2.12.2 Mapitio ya Mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Mwaka 2007/08, maeneo ya kipaumbele katika shughuli za Biashara Ndogo na za Kati yalikuwa yafuatayo:-

- i. Kujenga mazingira mazuri ya sheria na taratibu ili kuchochea uanzishwaji na ukuaji wa biashara;
- ii. Kuimarisha ujasiriamali, masoko na huduma;
- iii. Kuboresha fursa za upatikanaji mitaji kwa biashara ndogo na za kati;
- iv. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za kuendeleza sekta katika nyanja za teknolojia, masoko, upatikanaji wa taarifa na uendelezaji ujasiriamali; na
- v. Kuimarisha mfumo wa taasisi wa kuendeleza sekta ya Biashara Ndogo na za Kati

b) Utekelezaji:

Katika mwaka 2007/08, utekelezaji katika maeneo ya kipaumbele ulikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Programu ya Kuendeleza Viwanda Vidogo na Biashara ndogo Vijijini ijulikanayo kama Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI) ilianza kutekelezwa;
- ii. Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA) uliendelea kutekelezwa;
- iii. Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) uliendelea kutekelezwa; na
- iv. Taratibu bora za upatikanaji wa maeneo ya kufanyia biashara, kuimarisha ajira kwa vijana, wanawake na walemavu zimeandaliwa.

2.13 Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA)

2.13.1 Utangulizi

MKURABITA ulianzishwa na serikali kwa lengo la kuhakikisha kuwa biashara na rasilimali za wanyonge zilizo kwenye sekta isiyo rasmi zinarasimishwa kuziwezesha kutambulika kisheria.

2.13.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya Kipaumbele

Katika mwaka 2007/08, maeneo ya kipaumbele yalikuwa yafuatayo:-

- i. Kuendelea kufanya tafiti katika sekta isiyo rasmi ili kubaini ukubwa wake na thamani yake, kanuni na taratibu za uendeshaji na shughuli zinazofanyika katika sekta isiyo rasmi;
- ii. Kufanya tafiti ili kubaini vikwazo na vivutio vya kufanya biashara katika sekta isiyo rasmi;
- iii. Kutekeleza Mradi wa utoaji wa hati za kumiliki ardhi vijijini;
- iv. Kuanzisha benki kumi za mazao katika wilaya 5 nchini;na
- v. Kuhamasisha uanzishaji wa vyama vya kuweka na kukopa ili kusaidia benki za mazao.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08 utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele ulikuwa:-

- i. Watanzania waliwezesha kutumia rasilimali ziliorasimishwa kama dhamana kwa ajili ya kujipatia mikopo kutoka katika taasisi za fedha;
- ii. Utaratibu rahisi, wenye gharama nafuu na mfumo shirikishi na endelevu wa urasimishaji ardhi vijijini na mijini kwa mujibu wa sheria uliandaliwa;
- iii. Mfumo wa mawasiliano kati ya masijala mbalimbali hasa zinazohusu ardhi, watu (raia) na biashara uliandaliwa ili kukusanya, kuhifadhi na kutoa taarifa sahihi kuhusu umiliki mali na uendeshaji biashara kuanzia ngazi ya Kijiji/Shehia hadi Taifa.
- iv. Kanuni za uanzishaji, uendeshaji na ufungaji wa biashara ziliendelea kurahisishwa;
- v. Mwongozo wa urasimishaji rasilimali na biashara kwa mujibu wa sheria ulikamilika; na
- vi. Vijiji 211 vilipatiwa vyeti vya ardhi na wananchi binafsi wapatao 3,940 walipatiwa hati za kimila za kumiliki ardhi.

2.14 Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania 2020

2.14.1 Utangulizi

Serikali inatekeleza Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania (Tanzania Mini – Tiger Plan 2020) ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuondoa umaskini na kufikia malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mpango huu unalenga kujenga mazingira ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa kuanzisha Maeneo Maalum ya Uwekezaji na kuyapatia miundombinu muhimu, na yenye uhakika kwa kutumia uzoefu wa mafanikio ya nchi za kusini mashariki mwa Asia.

2.14.2 Mapitio ya Mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika mwaka 2007/08, maeneo ya kipaumbele yafuatayo yalipangwa kutekelezwa: -

- i. Kuendelea na ujenzi wa Eneo Maalum la Uwekezaji "Benjamin William Mkapa Special Economic Zone (BWM – SEZ)";
- ii. Kuunda mamlaka ya kusimamia maeneo maalum ya uwekezaji;
- iii. Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Watanzania katika nchi zenye uzoefu wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji;
- iv. Kuanza ujenzi wa Kituo Maalum cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT - SEZ) katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam; na
- v. Kulitangaza Eneo Maalumu la Uwekezaji la Mabibo ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08, Mpango huu ulitekeleza shughuli zifuatazo: -

- i. Ujenzi wa miundombinu ya umeme, kliniki, Migahawa, maduka, na kituo cha ukusanyaji wa kodi katika eneo Maalum la Uwekezaji "Benjamin William Mkapa ulikamilika
- ii. Kuhamishwa kwa shughuli zilizopangwa kufanywa na Mamlaka ya Kusimamia Maeneo Maalum ya Uwekezaji zilihamishiwa "Export Processing Zone Authority";
- iii. Upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa Kituo Maalum cha Habari na Mawasiliano (ICT – SEZ) eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulikamilishwa. Baadhi ya wataalam walikwenda Mauritius kupata uzoefu wa jinsi ya kuanzisha na kuendesha Kituo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; na
- iv. Makubaliano ya Awali (MoU) yalitiwa saina kati ya Serikali ya Tanzania na kampuni ya Oji Paper pamoja na Marubeni Corporation za Japan kwa ajili ya uanzishwaji wa misitu kwa ajili ya kuvuna mbaob na biashara (Commercial afforestation), katika

mikoa ya Mtwara na Lindi. Aidha vitalu vya miche ya majaribio tayari vimeanzishwa Katika vijiji sita Kwenye mikoa hiyo.

Eneo la Pili: Uboreshaji wa Hali ya Maisha na Maendeleo ya Jamii

2.15 Sekta ya Elimu

2.15.1 Utangulizi

Katika mwaka 2007/08 Serikali ililenga katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na fursa sawa ya kujiunga na elimu ya msingi na sekondari, kwa vijana wakike na wakiume; na pia kupanua uwigo wa elimu ya juu, vyuo vya mafunzo na vile vya ufundi stadi na kuhakikisha kuwa wananchi wote wanajua kusoma na kuandika. Serikali iliendelea kushirikisha sekta binafsi katika kutekeleza programu za kuendeleza elimu ya msingi na ya sekondari, (MMEM II na MMES).

2.15.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika mwaka 2007/08, maeneo ya kipaumbele katika sekta ya elimu yalikuwa yafuatayo:-

- i. Kuendelea kuifanyia marekebisho mitaala ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu pamoja na kuboresha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia;
- ii. Kuajiri walimu wenye ujuzi na uwezo katika shughuli za ufundishaji;
- iii. Kuongeza na kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu yakiwemo mafunzo, ukarabati na ujenzi wa nyumba, maslahi na vitendea kazi;
- iv. Kukamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kuwaendeleza Walimu (TDMS);
- v. Kutekeleza awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II);

- vi. Kuendelea kutekeleza na kuimarisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari;
- vii. Kuboresha uwezo na ushiriki wa kamati za shule katika kupanga, kutekeleza na kusimamia utoaji wa elimu bora katika kila ngazi ya elimu ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji katika usimamizi wa mifuko ya elimu; na
- viii. Kurekebisha/kukarabati ukumbi wa Chimwaga - Chuo Kikuu cha Dodoma.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08, utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele ulikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Shule mpya za msingi 924 zilijengwa ambapo kati ya hizo, 860 ni za serikali. Aidha, mikondo 9,691 iliongezwa;
- ii. Walimu wapya 3,872 wa shule za sekondari za serikali walijajiriwa na hivyo kuwa na uwiano bora zaidi kati ya mwalimu kwa wanafunzi (kidato cha 1 - 4) kutoka 1:48 mwaka 2006 hadi 1:45 mwaka 2007;
- iii. Kwa kushirikisha wananchi, Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari umefanikisha ujenzi wa jumla ya shule mpya za sekondari 1,196;
- iv. Vyuo vya ualimu vitatu vilijengwa/vilianzishwa ambapo viwili kati ya hivyo ni vya serikali; na
- v. Ukarabati wa vyuo vikuu vya Dodoma, Mkwawa na Chang'ombe ulikamilika.

2.16 Sekta ya Afya

2.16.1 Utangulizi

Serikali iliendelea kuboresha huduma za afya katika maeneo ya vijijini na mijini. Katika kipindi cha mwaka 2007/08 maeneo mbalimbali ya kipaumbele yalitekelezwa.

2.16.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika mwaka 2007/08, maeneo ya kipaumbele katika sekta ya afya yalikuwa yafuatayo:-

- i. Kuendelea na juhudi za kupunguza vifo vya watoto wachanga na vya uzazi kwa akina mama;
- ii. Kuendelea na jitihada za kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano;
- iii. Kuendelea kuboresha huduma kwa wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;
- iv. Kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii;
- v. Kuendelea kuboresha huduma za tiba ya Kifua Kikuu; na
- vi. Kuendelea kuboresha utafiti na mafunzo ya wataalam.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08, utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele ulikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Shughuli za uhamasishaji juu ya ushauri nasaha na upimaji wa hiari ziliendelea ambapo Mpango wa Taifa wa Upimaji UKIMWI kwa Hiari ulizinduliwa;
- ii. Mkakati wa Pili wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha mwaka 2008 hadi 2012 uliandaliwa;
- iii. Vituo vya kutolea huduma za mama na mtoto viliongezeka kupitia Mkakati Kabambe wa Kupunguza Vifo vya Mama na Mtoto;
- iv. Kuendelea kudhibiti maambukizo mapya ya VVU kwa kuwalenga zaidi wanawake, vijana na makundi yaliyo hatarini zaidi;
- v. Kuimarisha mafunzo ya maafisa wauguzi na tabibu pamoja na upanuzi wa vyuo vya mafunzo ili kukidhi mahitaji ya watumishi;
- vi. Kuendelea kuimarisha hospitali Teule za wilaya na za Mashirika ya Dini.

2.17 Maji Safi na Maji Taka

2.17.1 Utangulizi

Katika kipindi cha mwaka 2007/08, juhudi zilielekezwa katika upanuzi na uboreshaji wa huduma za maji safi katika maeneo ya mijini na vijijini na maji taka mijini.

2.17.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika mwaka 2007/08, maeneo ya kipaumbele katika utoaji huduma za maji safi na maji taka yalikuwa yafuatayo:-

- i. Kuendelea na usambazaji wa huduma za maji katika miji ya Kahama na Shinyanga na vijiji vinavyozunguka mradi wa maji wa Ziwa Victoria;
- ii. Kuendelea kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji katika mabonde yote ya maji;
- iii. Kuimarisha udhibiti wa uchafuzi wa mazingira kwa kuhakikisha kuwa sheria za utunzaji mazingira zinafuatwa;
- iv. Kuanzisha Mtandao wa Udhibiti wa Ubora wa Maji utakaohusisha mabonde sita ya maji;
- v. Kuendelea na ukarabati na upanuzi wa mitambo ya maji ya Mto Ruvu na usambazaji wa miundombinu ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na miji midogo ya Bagamoyo na Kibaha;
- vi. Kuendelea na ukarabati wa Miradi mikubwa ya Maji Vijijini ya Lushoto, Chalinze, Maswa, Mugango/Kiabakari na Wanging'ombe;
- vii. Kuimarisha teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua na kusambaza katika wilaya zenye ukame. Lengo ni wilaya 33 ifikapo mwaka 2009;
- viii. Kuendelea kuchimba visima virefu na vifupi vipatavyo 600 kwa ajili upatikanaji endelevu wa maji safi na ya gharama nafuu;

- ix. Kuendelea kutekeleza Programu ya Maji Safi na Maji Taka Vijijini ili kuongeza huduma ya usambazaji wa maji safi kutoka asilimia 53 mwaka 2006 hadi asilimia 65 ifikapo mwaka 2009; na
- x. Kuboresha huduma za majitaka na kuongeza kiwango cha huduma hii kutoka asilimia 17 mwaka 2006 hadi 30 mwaka 2009.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08, utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele ulikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Utafiti ulifanyika katika mabonde tisa ili kutambua vyanzo vya maji kwa ajili ya kuvilinda na kuvihifadhi. Vyanzo vilivyotambuliwa viliwekewa mipaka na kupangwa katika kanda;
- ii. Mamlaka za maji zinazosimamia maji kwenye mabonde zilifanya utafiti unaohusu matumizi ya maji na utoaji vibali vya maji;
- iii. Sampuli 2,837 za mfumo wa maji safi ya bomba, visima, mito, chemchemi na maziwa zilikusanywa kwa ajili ya kufanyiwa utafiti wa kimaabara ili kugundua viwango vya kemikali na matokeo yake kupelekwa kwenye taasisi husika na ushauri wa kitaalamu ulitolewa;
- iv. Uchambuzi wa kimaabara wa sampuli za majitaka kutoka katika mabwawa ya kuhifadhi maji hayo ulifanywa katika miji ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma;
- v. Miradi mitano ya uvunaji wa maji ya mvua kwa kuweka matenki katika shule za msingi na miradi sita kama hiyo katika shule za sekondari za wilaya ya Bariadi mkoani Shinyanga ilikamilika.
- vi. Usanifu wa kina wa miradi 22 ya uvunaji wa maji ya mvua mkoani Pwani na maeneo ya pembeni mwa Dar es Salaam ulikamilika;
- vii. Utekelezaji wa miradi ya kijamii ya maji safi na majitaka katika wilaya za Hai na Moshi Vijijini iliyohusisha ukarabati na ujenzi wa skimu za usambazaji wa maji za Lyamungo na Mailisita

- wilayani Hai na ujenzi wa mabwawa saba ya kuhifadha maji (reservoirs) wilayani Moshi Vijijini uliendelea; na
- viii. Ujenzi wa mabwawa sita ya maji katika wilaya za Misungwi, Maswa, Bunda na Serengeti umekamilika.

Eneo la Tatu: Utawala Bora na Uwajibikaji

2.18 Utawala bora

2.18.1 Utangulizi

Katika mwaka 2007/08 Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya uchumi na taratibu kwa lengo la kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika kusimamia: rasilimali za umma, usalama wa raia, haki za binadamu, mifumo ya sheria na vita dhidi ya rushwa.

2.18.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika kipindi cha mwaka 2007/08, Serikali ilipanga kutekeleza yafuatayo:-

- i. Kuratibu utekelezaji wa masuala ya Utawala Bora hususan Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali pamoja na Mashirika ya Umma na Taasisi;
- ii. Kupanua wigo wa mapambano ya vita vya rushwa nchini kwa kushirikisha asasi za kiraia na wadau wengine katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa;
- iii. Kuendelea kudhibiti mianya ya rushwa katika utoaji wa huduma kwa umma; na
- iv. Kuelimisha umma kuhusu mapambano na vita dhidi ya rushwa.

b) Utekelezaji

Katika kipindi cha mwaka 2007/08, utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa ulikuwa kama ifuatavyo:

- i. Wajumbe 300 wa Kamati za Uadilifu zilizoundwa katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali pamoja na Mashirika na Taasisi walipewa mafunzo kwa ajili ya kuwawezesha kuratibu masuala ya Utawala Bora katika sehemu zao za kazi;
- ii. Ilitungwa Sheria Na. 11 ya mwaka 2007 ambayo imeongeza makosa ya rushwa kutoka manne chini ya Sheria Na. 16 ya mwaka 1971 hadi makosa 24 katika sheria hii mpya;
- iii. Matokeo na viashiria vya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa viliainishwa; na
- iv. Uteuzi wa wajumbe wa Kamati za Uadilifu katika sekta zote za umma uliendelea kufanyika.

2.19 Vita Dhidi ya UKIMWI

2.19.1 Utangulizi

Katika mwaka 2007/08 serikali iliweka msisitizo katika kuzuia maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARVs) kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI; na kuboresha mifumo na taratibu za usambazaji/ugawaji wa dawa hizo.

2.19.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya kipaumbele

Katika kupambana na UKIMWI mwaka 2007/08 serikali ilipanga kutekeleza yafuatayo:-

- i. Kudhibiti kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI nchini;
- ii. Kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI toka kwa mama kwenda kwa mtoto;

- iii. Kushirikisha viongozi wa kisiasa, madhehebu ya dini, taasisi za umma na watu binafsi katika kupunguza unyanyapaa;
- iv. Kuelimisha umma juu ya maambukizi na njia sahihi za kujikinga na VVU na magonjwa ya zinaa; na
- v. Kutoa matunzo na misaada kwa idadi kubwa zaidi ya watu waishio na VVU/UKIMWI katika ngazi za majumbani, jumuiya hadi hospitali.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08, utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Mafunzo yalitolewa katika sehemu za kazi kwa makundi mbalimbali, pamoja na huduma kama kupima UKIMWI kwa hiari na madawa ya kupunguza makali kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI;
- ii. Uelimishaji jamii katika jumuiya za walioathirika na madawa ya kulevya ulifanyika;
- iii. Kamati za UKIMWI katika baadhi ya sehemu za kazi zilianzishwa, pamoja na uelimishaji rika; na
- iv. Programu ya kitaifa kwa ajili ya kupambana na magonjwa nyemelezi kama vile kifua kikuu na Malaria nayo ilianzishwa.

2.20 Mazingira

2.20.1 Utangulizi

Serikali iliendelea kutekeleza Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, ambao ulipitishwa 2006. Mkakati huu umeainisha changamoto kadhaa kuhusu uharibifu wa mazingira nchini, maeneo yaliyoharibika, hatua na mikakati ya utekelezaji.

2.20.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya Kipaumbele

Katika mwaka 2007/08, maeneo yaliyopewa kipaumbele yalikuwa:

- i. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mazingira na mikakati yake na kukuza weledi juu ya uhusiano kati ya mazingira, umaskini na maendeleo endelevu;
- ii. Kutekeleza mikakati, programu na miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira; na
- iii. Kutekeleza mikataba na itifaki za kikanda na kimataifa zinazohusu hifadhi ya Mazingira.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08, utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira ulisambazwa nchini kote, na kufuatilla utekelezaji wake katika wizara mbalimbali;
- ii. Kanuni mbalimbali za hifadhi ya mazingira ziliandaliwa, zikiwemo Kanuni za Viwango vya Ubora wa Mazingira, Kanuni za Ada na Tozo, Kanuni kuhusu Kemikali zinazoharibu Tabaka la Ozoni na Kanuni za Tathmini ya Kimkakati ya Athari ya Mazingira;
- iii. Ripoti ya Hali ya Mazingira iliandaliwa ambayo imeainisha maeneo muhimu ki-sekta na hatua za kuchukua kila ngazi;
- iv. Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Bonde la Mto Nile uliendelea kutekelezwa, ambapo mafunzo kwa wadau mbalimbali kuhusu hifadhi ya mazingira yalitolewa;
- v. Maandalizi ya Ripoti ya pili ya utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi yalianza, ambapo uchambuzi wa kina wa athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika sekta za kilimo, afya na maji ulikamilika;
- vi. Miradi 50 ilifanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira na kupatiwa vyeti kwa ajili ya utekelezaji;

- vii. Taarifa ya tatu ya Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa kuhusu Hifadhi ya Bioanuai iliandaliwa;
- viii. Mwongozo kuhusu usimamizi wa bidhaa na viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki ulikamilika.
- ix. Chini ya Mkataba wa Montreal unaohusu Udhibiti wa Kemikali zinazoharibu Tabaka la Hewa ya Ozoni, Rasimu ya Mwongozo wa namna ya kuhudumia viyoyozi na majokofu ilikamilishwa na warsha ya mafunzo kwa mafundi mchundo 30 wa viyoyozi na majokofu ilifanyika katika Kanda ya Kusini;

2.21 Jinsia

2.21.1 Utangulizi

Serikali imeendelea kuandaa, kufuatilia na kuwezesha utekelezaji wa Sera mbalimbali zinazolenga kuleta maendeleo ya jamii kwa kuzingatia uwiano wa kijinsia. Hii ni pamoja na kujenga mazingira pevu (condusive environment) yatakayoipa jamii uwezo wa kutambua na kutatua matatizo yanayoikabili.

2.21.2 Mapitio ya Mwaka 2007/08

a) Maeneo ya Kipaumbele

Katika kutekeleza shughuli za jinsia serikali mwaka 2007/08 iliweka kipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

- i. Kuendelea kujenga uwezo wa namna ya kutungamanisha masuala ya jinsia kwenye mipango katika ngazi zote;
- ii. Kuanzisha utaratibu wa kufanya tathmini na usimamizi wa shughuli za jinsia;
- iii. Kuimarisha vikundi vya wanawake vya ushirika vya kuweka na kukopa (SACCOS) na vikundi vya maendeleo vya wanawake;
- iv. Kuimarisha mahusiano ya kijinsia katika ngazi zote; na

- v. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake katika Halmashauri 121 na kutoa stadi za ujasiriamali kwa wanawake.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08, utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo :-

- i. Mafunzo kuhusu kutungamanisha masuala ya jinsia katika mipango ya wilaya yalitolewa kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Mipango wa Wilaya kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara;
- ii. Mafunzo ya ujasiriamali yalitolewa kwa wanawake 3,000 kutoka katika mikoa ya Pwani, Iringa, Dar es Salaam, Mtwara na Lindi.
- iii. Wanawake wajasiriamali 54 waliwezesha kushiriki maonesho ya Kimataifa ya biashara ya Dar es salaam;
- iv. Wanawake 200 wakiwemo askari Mageraza, Polisi na Mahakama toka mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara, Tanga na Dar es salaam walielimishwa kuhusu sheria za ndoa, mirathi pamoja na Sheria ya Ardhi Na 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999;
- v. Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ulitoa kiasi cha shilingi 464 milioni kwenda kwenye Halmashauri 133 ili ziweze kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya Wanawake;
- vi. Halmashauri 35 zilitoa mafunzo ya ujasiriamali na stadi za kazi kwa vikundi vya wanawake waliokopeshwa fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake kwenye Halmashauri zao; na
- vii. Mchakato wa kuwezesha uanzishwaji wa Benki ya Wanawake unaendelea ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa ununuzi wa hisa.

2.22 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

2.22.1 Utangulizi

Serikali kwa mwaka 2007/08 ililenga kutekeleza sera ya Taifa ya Uwezeshaji pamoja na kutekeleza mikakati mbali mbali ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

2.22.2 Mapitio ya Mwaka 2007/08

a) Maeneo ya Kipaumbele

Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2007/08 yalikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Kusimamia utekelezaji wa sera ya Taifa ya Uwezeshaji;
- ii. Kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (Mwananchi Economic Empowerment Fund);
- iii. Kutoa mafunzo kwa watendaji wa Benki na maafisa wa serikali wanaohusika na masuala ya uwezeshaji;
- iv. Kufuatilia na kutathmini programu ya fedha za Uwezeshaji; na
- v. Kuhamasisha wananchi kuhusu mpango na programu za uwezeshaji.

b) Utekelezaji

Katika kutekeleza mpango huu, Benki kuu ya Tanzania ilitoa mafunzo yanayohusu dhana ya uwezeshaji kwa maafisa 277 kutoka benki mbalimbali, maafisa 774 kutoka manispaa mbalimbali za miji, na maafisa 29 wa SCCULT;

- i. Katika awamu ya kwanza Mfuko wa Dhamana wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira ulitoa mikopo kwa wajasiriamali 38,097 yenye thamani ya sh. 31.7 bilioni kupitia benki za NMB na CRDB, ikiwa ni zaidi ya lengo kwa sh. 0.2 bilioni;
- ii. Katika awamu ya pili, serikali ilitenga sh. 10.5 bilioni kwa ajili ya kuendelea kutoa mikopo. Aidha, benki na asasi za kifedha za

kutoa mikopo ziliongezeka. Benki na asasi hizo ni: Akiba Commercial Bank (ACB); Benki ya Posta; Kagera Farmers Cooperative Bank Ltd; Kilimanjaro Cooperative Bank; SCCULT (1992) Ltd; Benki ya Wananchi Mbinga; Pride Tanzania; Benki ya Wananchi Mufindi; Azania Bank; Shirika la Dunduliza; Uchumi Commercial Bank; Presidential Trust Fund; na Benki ya Wananchi Mwanga; na

- iii. Wananchi wengi walihamasishwa na kuelimishwa kuhusu mpango na programu za uwezeshaji kiuchumi.

2.23 Ajira

2.23.1 Utangulizi

Pamoja na kupungua kwa ukosefu wa ajira kutoka asilimia 12.9 mwaka 2000/01 kufikia asilimia 11.0 mwaka 2005/06, tatizo la ukosefu wa ajira hapa nchini limeendelea kuwa changamoto. Kutokana na hali hii mipango mbalimbali imekuwa ikitekelezwa na serikali pamoja na wadau wengine ili kupunguza tatizo hili.

2.23.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya Kipaumbele

Katika kipindi cha mwaka 2007/08 serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Kukuza Ajira ulioanza mwaka 2006 ambapo maeneo ya kipaumbele yalikuwa yafuatayo:-

- i. Kukamilisha na kuanza kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira na mkakati wake;
- ii. Kuteleleza Programu ya Taifa ya Kuongeza Ajira;
- iii. Kuendelea kufanya kaguzi sehemu za kazi hususan kwenye Viwanda na makampuni binafsi kwa lengo la kufuatilia kama waajiri wanafuata sheria na taratibu za nchi kuhusu ajira;
- iv. Kuratibu ushiriki wa wajasiriamali wadogo wa sekta isiyo rasmi nchini katika maonesho ya tisa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Nguvukazi/Jua Kali Nairobi Mwezi Oktoba 2008;

- v. Kuendelea kutekeleza mpango wa mafunzo ya kuwawezesha wananchi kujiajiri; na
- vi. Kuendelea kupanua huduma za ajira nchini kwa kufungua vituo vipya vya ajira.

b) Utekelezaji

Katika mwaka 2007/08, utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele ulikuwa kama ifuatavyo:

- i. Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008 imepitishwa na Mkakati wa Taifa wa Ajira kwa ajili ya kutekeleza sera umeandaliwa;
- ii. Utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kukuza Ajira umeendelea ambapo kufikia Novemba 2007, zaidi ya nafasi mpya za ajira 401,390 zilikuwa zimepatikana katika sekta mbalimbali;
- iii. Wajasiriamali wadogo wa sekta isiyo rasmi wapatao 209 walishiriki katika maonesho ya tisa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Nguvu kazi/Jua Kali Nairobi Mwezi Oktoba 2008
- iv. Halmashauri tisa zilipatiwa mafunzo ya kuwawezesha wananchi kujiajiri na kupunguza umaskini;
- v. Mazingira ya kazi kwa wajasiriamali katika sekta isiyo rasmi yaliboreshwa, na ujenzi wa sehemu ya kufanyia shughuli (Business Parks) kwa wajasiriamali wa sekta isiyo rasmi Jijini Dar es Salaam ulianza;
- vi. Kituo cha ajira (Labour Exchange Centre) kilianzishwa mkoani Mwanza ili kutoa huduma kwa wakazi wa kanda ya ziwa.

2.24 Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

2.24.1 Utangulizi

Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaendelea kuwa vyombo muhimu katika utekelezaji wa Sera, mikakati, programu na miradi mbalimbali ili kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii. Jukumu hili linatekelezwa kupitia mfumo wa uboreshaji wa Serikali za mitaa na hasa utekelezaji wa Sera ya Upelekaji wa Madaraka kwa Wananchi.

2.24.2 Mapitio ya mwaka 2007/08

a) Maeneo ya Kipaumbele

Mikoa na Serikali za Mitaa zilianisha maeneo yafuatayo kuwa ya kipaumbele kwa mwaka 2007/08:-

- i. Ukarabati wa Hospitali za Mikoa ya Tabora, Kigoma, Tanga, Shinyanga, Singida, Lindi, Ruvuma, Rukwa, Dodoma, Mara na Iringa ;
- ii. Kujenga ofisi za wakuu wa Wilaya na nyumba za kuishi kwa ajili ya Wilaya mpya.
- iii. Kuwezesha uanzishaji wa Mipango ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya Halmashauri
- iv. Ujenzi na ukarabati wa makao makuu kwa Halmashauri mpya
- v. Ujenzi na ukarabati wa ofisi za kata.

b) Utekelezaji

Katika kipindi cha mwaka 2007/08 utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele katika Mikoa na Halmashauri ulikuwa kama ifuatavyo:-

- i. Hospitali za Mikoa ya Tabora, Kigoma, Tanga, Shinyanga, Singida, Lindi, Ruvuma, Rukwa, Dodoma, Mara na Iringa zilikarabatiwa;
- ii. Ofisi na nyumba za kuishi wakuu wa wilaya mpya zilijengwa;
- iii. Ujenzi wa ofisi ya mkuu wa Mkoa wa Manyara ulikamilishwa;
- iv. Ujenzi/Ukarabati wa ofisi za Halmashauri za Sumbawanga, Korogwe, Babati, Mpanda, Karatu, Mvomero, Kilindi, Kishapu, Namtumbo, Kilolo, Ruangwa, Bahi, Misenyi, Chato, Longido, Ukerewe, Rorya, Mbarali, Mkuranga, Pangani, Misungwi, Meru, Nanyumbu, na Siha ulikamilika; na
- v. Ujenzi na Ukarabati wa nyumba za watumishi wa Halmashauri za Ruangwa, Ngorongoro na Mahenge uliendelea.

SURA YA TATU
MADHUMUNI , MWELEKEO, CHANGAMOTO NA UTEKELEZAJI
WA MKUKUTA KATIKA MPANGO WA MWAKA 2008/09

3.1 Madhumuni na Mwelekeo

Serikali imetayarisha Mpango wa Mwaka 2008/09 ambao unatoa tafsiri ya maagizo mbalimbali ya Serikali na malengo ya Ilani ya CCM ya uchaguzi wa Mwaka 2005. Mpango huu ni wa nne katika utekelezaji wa MKUKUTA, ambao ni Mkakati wa kutekeleza Malengo ya Dira ya Maendeleo 2025 na maagizo ya Ilani ya CCM ya uchaguzi ya mwaka 2005. Mambo muhimu yanayosisitizwa ni :- kuleta maisha bora, kuendeleza amani na utulivu kwa kuzingatia utawala bora na uwajibikaji.

Mpango huu umeandaliwa kwa kuangalia upatikanaji wa matokeo ya mambo yanayosisitizwa hapo juu. Ili kufanikisha hayo tunahitajika kuwa makini zaidi katika upangaji wa vipaumbele na rasilimali; pamoja na kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji ili rasilimali chache tulizonazo zitumike kwa ufanisi. Jambo muhimu linalojitokeza katika Mpango huu ni kuendeleza uamuzi wa serikali wa kugawa rasilimali za kutosha katika maeneo machache yatakayokamilishwa kwa muda mfupi na kuleta msukumo katika ukuaji wa uchumi.

Utekelezaji wa uamuzi huu utaendelea kusioniwa kwa kupitia upya mfumo wa bajeti zinazoandaliwa na Wizara, Mikoa, Taasisi na Serikali za Mitaa. Hatua zimeanza kuchukuliwa kwa kuangalia shughuli zote zinazopangwa na watekelezaji na kuona kama zinaoana vizuri na maamuzi haya pamoja na majukumu makuu ya taasisi husika. Aidha, hatua hii inategemewa kuondoa migongano katika utekelezaji na kuendelea kuratibu shughuli zote zinazotekelezwa na Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa zinazochangia katika matokeo. Vile vile, rasilimali

zitaelekezwa katika maeneo yatakayoleta matokeo na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Mpango utaendelea kuimarisha mafanikio yaliyopatikana katika utoaji wa huduma za jamii hasa katika elimu ya msingi, sekondari, na afya ya msingi kwa kupewa rasilimali za kutosha.

3.2 Changamoto

Changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2008/09 ni pamoja na:-

- i. Kuhakikisha kwamba vipaumbele vya kitaifa vinaeleweka katika ngazi zote ili viweze kutekelezwa hatua kwa hatua na kuleta matokeo yaliyokusudiwa kwa wakati uliopangwa;
- ii. Kuwa na mapato yatakayoweza kukidhi mahitaji ya vipaumbele, kwa kuendelea kuboresha mfumo wa makusanyo ikiwa ni pamoja na kurekebisha sheria zinazohusu makusanyo yote ya Serikali; na kuhakikisha kuwa yanaingia kwenye mfuko mkuu wa Serikali hasa mapato yanayokusanywa na wakala wa Serikali pamoja na Idara nyingine za Serikali;
- iii. Kuendelea kuimarisha utaratibu wa ugawaji wa rasilimali kulingana na vipaumbele vya MKUKUTA na Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa mwaka 2005;
- iv. Kuendelea kuboresha mazingira ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje;
- v. Kuzipa uwezo Serikali za Mitaa ili ziweze kutekeleza kwa ufanisi maamuzi ya kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia serikali zao kwa maana ya kuajiri, kutoa mafunzo na nyenzo za kufanyia kazi; na
- vi. Kukabiliana na mahitaji mengi ya matumizi kuliko uwezo wa mapato ya Serikali na kusimamia miongozo inayotolewa hususan ya mipango na bajeti.

3.3 Utekelezaji wa MKUKUTA katika mwaka 2008/09

Katika mwaka 2008/09, Serikali itaendelea kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali inayolenga kukuza uchumi na kupunguza umaskini na kuleta ustawi wa jamii. Ili kufanikisha malengo hayo, utayarishaji wa mipango na programu mbalimbali za maendeleo ya kisekta na mikoa unazingatia maeneo makuu matatu ya MKUKUTA ambayo ni Ukuaji Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato; Uimarishaji wa Hali ya Maisha na Maendeleo ya Jamii; na Utawala Bora na Uwajibikaji.

Eneo la Kwanza: Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umaskini wa Kipato

3.3.1 Sekta ya Kilimo

a) Utangulizi

Katika kutekeleza malengo ya MKUKUTA na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 Serikali kwa mwaka 2008/09 itaendelea kutekeleza mipango na programu ambazo zinalenga katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini ili kuwavutia wawekezaji wengi katika sekta ya kilimo, kupanua kilimo cha umwagiliaji, upatikanaji wa mbolea, madawa ya kuulia wadudu na huduma za ugani kwa wakulima kwa wakati muafaka.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Mwaka 2008/09, maeneo ya kipaumbele katika sekta ya kilimo yatakuwa yafuatayo:

- i. Kuzijengea Sekretarieti za Mikoa uwezo wa kuzisaidia Halmashauri za Wilaya kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs);
- ii. Kuimarisha mipango na programu zitakazoweza kuhakikisha usalama wa chakula na kukua kwa pato la mkulima;

- iii. Kuboresha huduma mbalimbali za kilimo na shughuli za usimamizi wa kisera;
- iv. Kuendelea kuandaa Mikakati wa Matumizi bora ya Ardhi;
- v. Kuimarisha mikakati ya kuongeza idadi ya wawekezaji binafsi katika sekta ya kilimo;
- vi. Kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara;
- vii. Kuwafundisha wakulima matumizi ya vifaa mbalimbali vya umwagiliaji katika sehemu mbalimbali ambapo kilimo cha umwagiliaji kinafanyika; na
- viii. Kuviwezesha vyama vya wazalishaji kuzalisha mazao ambayo yanakidhi matakwa ya soko la ndani na nje.

c) Mikakati

Ili kufanikisha utekelezaji katika maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa, mikakati itakayotumika mwaka 2008/2009, ni kama ifuatavyo:-

- i. Kujenga miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao kutokana na kilimo cha umwagiliaji;
- ii. Kuwajengea uwezo maafisa kilimo ili kutoa huduma za kiutaalam kwa wakulima;
- iii. Kuongeza shughuli za sekta ya umma na binafsi katika uimarishaji wa huduma za kilimo;
- iv. Kusambaza kwa wakati pembejeo za kilimo kwa wakulima na vyama vya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara; na
- v. Kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kote nchini.

3.3.2 Sekta ya Mifugo

a) Utangulizi

Mchango wa sekta ndogo ya mifugo utalenga katika upatikanaji wa chakula na lishe, nguvu kazi wanyama, usafirishaji, biashara, mbolea ya samadi kwa kilimo endelevu na utoaji wa nishati.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Katika mwaka 2008/09 maeneo muhimu ya utekelezaji yatakuwa yafuatayo:

- i. Kuimarisha ukusanyaji, utunzaji, na matumizi ya takwimu sahihi za mifugo pamoja na usambazaji wa matokeo ya tafiti mbalimbali kwa wadau;
- ii. Kujenga na kuimarisha miundombinu mbalimbali ya mifugo kama majosho na malambo;
- iii. Kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya mifugo;
- iv. Kuimarisha uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine wanaotoa huduma za mifugo;
- v. Kuongeza tija na kuboresha usindikaji, masoko ya bidhaa za mifugo na mifumo ya malisho;
- vi. Kuongeza ubora wa pembejeo za mifugo, mazao ya mifugo na huduma za ukaguzi; na
- vii. Kuandaa na kutekeleza mpango wa kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya mifugo.

c) Mikakati

Utekelezaji katika mwaka 2008/09 utazingatia mikakati ifuatayo:

- i. Kuhimiza sekta binafsi kushiriki katika uzalishaji, usindikaji na uuzaji nje wa bidhaa za mifugo na mifugo ya ziada;
- ii. Kuhamasisha halmashauri kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo ambao utatumika kugharamia chanjo za mifugo;
- iii. Kuanzisha mpango kabambe ambao utagharamiwa na Serikali kudhibiti ugonjwa wa homa ya mapafu;
- iv. Kujenga malambo yatakayohifadhi maji kwa kipindi kirefu kwa ajili ya mifugo na kuendeleza sehemu za malisho;
- v. Serikali na sekta binafsi kuimarisha huduma za ugani na utafiti ili kuendeleza sekta ya mifugo;

- vi. Kuanzisha vyama vya wafugaji na vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa katika maeneo ya wafugaji;
- vii. Kutoa taarifa za masoko mazuri ya bidhaa za mifugo kwa wadau; na
- viii. Kuhamasisha benki za biashara kutoa mikopo kwa sekta ya mifugo.

3.3.3 Ushirika na Masoko

a) Utangulizi

Mwaka 2008/09 sekta hii italenga katika uzalishaji wa mazao na kuongeza nguvu ya umiliki wa soko kwa ufanisi zaidi.

b) Mpango kwa Mwaka 2008/09

Katika mwaka 2008/09 maeneo ya kipaumbele katika sekta ya ushirika na masoko ni kama ifuatavyo:

- i. Kuboresha upatikanaji wa mikopo ya uendelezaji wa ushirika na masoko katika ngazi zote;
- ii. Kuimarisha shughuli za ushirika na masoko ili kuongeza pato la wananchi;
- iii. Kuongeza upatikanaji wa masoko kwa mazao ya chakula na biashara na kuyatumia kikamilifu; na
- iv. Kuongeza ubora wa bidhaa ili kuongeza ushindani katika mfumo wa masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi.

c) Mikakati

Utekelezaji katika mwaka 2008/09 utazingatia mikakati ifuatayo:-

- i. Kuandaa mazingira mazuri ya shughuli za biashara ili kupata soko la uhakika kwa mazao ya kilimo;
- ii. Kuongeza shughuli za sekta ya umma na binafsi katika kuimarisha huduma za ushirika na masoko;
- iii. Kuboresha usimamizi wa masoko ikiwa ni pamoja na kutayarisha na kusambaza takwimu na taarifa zilizochambuliwa za shughuli za ushirika na masoko; na

- iv. Kuhamasisha wadau kuanzisha vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa ili kuongeza upatikanaji wa mitaji midogo na ya kati.

3.3.4 Barabara

a) Utangulizi

Sekta ndogo ya barabara inalenga kuwa na mtandao wa barabara zinazopitika katika kipindi chote cha mwaka. Katika mwaka 2008/09, kipaumbele cha sekta hii ni kuhakikisha kuwa mikataba yote ya miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara inayoendelea inakamilishwa kwa wakati na ubora unaotakiwa.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Maeneo ya kipaumbele katika sekta ndogo ya barabara mwaka 2008/09 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kutekeleza programu ya maendeleo na ukarabati wa miundombinu hususan miradi inayoendelea ya barabara kuu, barabara za mikoa na barabara muhimu za vijijini;
- ii. Kuratibu usalama na utunzaji wa mazingira katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu; na
- iii. Kutekeleza Programu ya Uwekezaji katika Miundombinu ya Uchukuzi.

c) Mikakati

Utekelezaji katika mwaka 2008/09 utazingatia mikakati ifuatayo:-

- i. Kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kudumisha na kukarabati miundombinu iliyopo, na kujenga miundombinu mipya;
- ii. Kuanzisha njia endelevu za kugharamia na kudumisha miundombinu;
- iii. Kuzijengea uwezo wakala zote zinazohusika na maendeleo ya miundombinu;

- iv. Kuwahamasisha wananchi wa vijijini kufanya shughuli za ujenzi, ukarabati na udumishaji wa miundombinu kwa kutumia rasilimali za ndani na teknolojia ya kutumia wafanyakazi;
- v. Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli mbalimbali za kuendeleza miundombinu;
- vi. Kuongeza upatikanaji wa mitambo na vifaa vya ujenzi wa barabara ili kutengeneza soko shindani la ukodishaji; na
- vii. Kuimarisha matumizi ya teknolojia sahihi katika ujenzi na udumishaji wa barabara.

3.3.5 Mawasiliano na Uchukuzi

a) Utangulizi

Katika mwaka 2008/09 sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi imeweka mkazo kwenye ushirikishawaji wa sekta binafsi katika uendeshaji na utoaji huduma mbalimbali za mawasiliano na uchukuzi.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Maeneo ya kipaumbele ya sekta ndogo ya mawasiliano na uchukuzi kwa mwaka 2008/09 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kutekeleza Programu ya Maendeleo na Ukarabati wa Miundombinu;
- ii. Kuimarisha na kupanua Kitengo cha Makontena, na mlango wa bahari wa kuingilia katika bandari ya Dar es Salaam;
- iii. Kukarabati Reli ya Kati, kati ya Dar es Salaam na Morogoro;
- iv. Kukarabati na kununua vivuko;
- v. Kununua vifaa vya kupima hali ya hewa; na
- vi. Kuratibu usalama na utunzaji wa mazingira katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu.

c) Mikakati

Utekelezaji katika mwaka 2008/09 utazingatia mikakati ifuatayo:-

- i. uongeza usajili wa wanafunzi katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ili kuondoa tatazo la wataalam wa ICT na STI hapa nchini;
- ii. Kuboresha mtandao wa habari, mawasiliano na sayansi kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi;
- iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ili kuboresha utoaji wa huduma; na
- iv. Kuandaa na kuzi-maistream ajenda za ICT na STI katika sekta zote za uchumi nchini.

3.3.6 Ardhi

a) Utangulizi

Katika mwaka 2008/09 Serikali inalenga kuboresha makazi katika miji kwa kupunguza kasi ya ujenzi holela, kuongeza kasi ya upimaji wa viwanja vipya na mipaka ya vijiji, wilaya, mikoa na taifa.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Katika mwaka 2008/09 maeneo ya kipaumbele katika sekta ya ardhi ni:-

- i. Kuendelea kutoa barua za toleo na hati za kumiliki ardhi;
- ii. Kuboresha taarifa za Geo nchini; na
- iii. Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa nyumba bora na maendeleo endelevu ya makazi ya binadamu.

c) Mikakati

Utekelezaji katika mwaka 2008/09 utazingatia mikakati ifuatayo:-

- i. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa sheria za ardhi na sera husika;

- ii. Kuboresha michakato ya kutoa huduma hususan kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye maeneo ya upatikanaji wa vifaa, rasilimali watu na fedha;
- iii. Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuendeleza miji kwa kuzingatia mipango mikuu iliyopo; na
- iv. Kuboresha ukusanyaji wa kodi za ardhi.

3.3.7 Sekta ya Nishati

a) Utangulizi

Katika mwaka 2008/09 Serikali inalenga kuwapatia wananchi walio wengi hususan wanaoishi vijijini nishati endelevu na ya uhakika.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2008/09 ni kama yafuatavyo:-

- i. Kuendelea kusambaza umeme ili uwafikie wananchi walio wengi hususan wanaoishi vijijini;
- ii. Kuendeleza, kuimarisha na kupanua mfumo wa miundombinu ya nishati;
- iii. Kukamilisha uanzishwaji wa Mkakati Maalum wa Akiba ya Petroli na Biashara nchini; na
- iv. Kuendeleza tafiti mbalimbali za upatikanaji wa nishati endelevu na zenye uhakika.

c) Mikakati

Ili kufanikisha utekelezaji katika maeneo ya kipaumbele yaliyowekwa katika sekta ya nishati, mikakati ifuatayo itazingatiwa:-

- i. Kufanya matengenezo ya mitambo ya umeme;
- ii. Kuhamasisha wawekezaji binafsi katika sekta ya nishati;
- iii. Kutekeleza miradi ya maendeleo ya nishati kwa lengo la kuongeza wigo wa upatikanaji wa nishati nchini;

- iv. Kuimarisha njia za umeme zenye msongo mkubwa (high voltage), kuimarisha usambazaji na kuongeza vituo vidogo vya umeme;
- v. Kuendeleza na kuhuisha vyanzo vya nishati mbadala; na
- vi. Kuendelea kuwekeza katika miradi ya Songo Songo na Mnazi Bay.

3.3.8 Sekta ya Madini

a) Utangulizi

Serikali inazingatia pamoja na mambo mengine kuwapa uwezo Wachimbaji Wadogo na wa Kati kwa kuwapatia teknolojia iliyo bora na kuongeza thamani ya madini kabla ya kuyauza nchi za nje.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Maeneo ya kipaumbele katika sekta ya madini kwa mwaka 2008/09 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuhamasisha maendeleo ya uwekezaji katika sekta ya madini;
- ii. Kuongeza thamani ya madini ili kuongeza mapato yatoakanayo na uuzaji wa madini;
- iii. Kuboresha mazingira na kuendeleza wachimbaji wadogo na wa Kati;
- iv. Ujenzi wa maghala ya kuhifadhi udongo wa madini (cores from exploration) kwa ajili ya makampuni ya Madini.

c) Mikakati

Mikakati ya utekelezaji kwa mwaka 2008/09 ni pamoja na:-

- i. Kufanya marekebisho ya Sera ya Madini ya mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya mwaka 1998;
- ii. Kuendelea kufanya majadiliano na makampuni ya madini kwa lengo la kuhakikisha wadau wanafaidika;
- iii. Kuendelea kutumia taarifa za upatikanaji madini ili kuepusha tatizo la kutoa leseni ya umiliki kwa zaidi ya mmiliki mmoja; na

- iv. Kuendelea kuboresha mazingira ya kuongeza thamani ya madini kabla ya kuyauza nchi za nje.

3.3.9 Maliasili na Utalii

a) Utangulizi

Katika mwaka 2008/09, serikali inalenga kuboresha, kulinda, kuhifadhi na kuvuna kiendelevu rasilimali za maliasili na malikale pamoja na kuzingatia sheria na kanuni zinazosimamia biashara na uwekezaji katika sekta hizo pamoja na utalii.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Maeneo ya kipaumbele katika sekta ya maliasili na utalii kwa mwaka 2008/09 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuimarisha ushirikishwaji wa wadau katika usimamizi na matumizi endelevu ya maliasili;
- ii. Kuongeza mapato yatokanayo na maliasili, utamaduni na utalii;
- iii. Kupunguza vitendo haramu kwenye rasilimali za mali asili na utalii;
- iv. Kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika rasilimali samani na rasilimali fedha.

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatavyo:-

- i. Kurekebisha na kuhuisha sheria mbalimbali zinazohusu usimamizi na uendelezaji wa maliasili, malikale na biashara ya utalii.
- ii. Kuratibu na kufuatilia matumizi ya rasilimali na ukusanyaji mapato.
- iii. Kutekeleza malengo ya MKUKUTA yaliyoainishwa katika sekta ya maliasili na utalii.

3.3.10 Viwanda na Biashara

a) Utangulizi

Katika mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza programu maalumu ya uzalishaji wa bidhaa za kuuza nje. Aidha, Serikali inalenga kutekeleza mikakati ya kuimarisha uhusiano wa kibiashara na uwezeshaji na China pamoja na nchi nyingine za Asia na Mashariki ya Kati.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Maeneo ya kipaumbele katika sekta ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2008/09 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuimarisha maendeleo ya Viwanda Vidogo na vya Kati na kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwa kusindika bidhaa za kilimo;
- ii. Kuendelea kutekeleza Mchango wa Sekta za Kiuchumi Katika kukuza Mauzo (Diagnostic Trade Intergration Study – DTIS);
- iii. Kuvutia wawekezaji katika uzalishaji, kuongeza upatikanaji wa soko na kuboresha teknolojia za biogas, kusindika bidhaa za kilimo, na mionzi ya jua;
- iv. Kuimarisha Taasisi za Maendeleo zinazojihusisha na Utafiti;
- v. Kutoa mafunzo ya ujasiriamali; na
- vi. Kuendelea kutekeleza programu ya MKUMBITA na sheria ya Ushindani ya mwaka 2003.

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i. Kurejea na kuendeleza utekelezaji wa "Basic Industry Strategy (BIS)" ikiainishwa na Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda;
- ii. Kubainisha maeneo kwa ajili ya kuendeleza viwanda, biashara na masoko katika mikoa;

- iii. Kuhamasisha uwekezaji kwenye miundombinu katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuendeleza viwanda na biashara;
- iv. Kutoa mafunzo katika fani mbalimbali kwa wajasiriamali; na
- v. Kuendeleza utekelezaji wa Sheria ya kuanzishwa Maeneo Maalumu ya Uuzaji Bidhaa Nje.

3.3.11 Biashara Ndogo na za Kati (SMEs)

a) Utangulizi

Serikali imekuwa ikihamasisha uanzishaji na uendelezaji wa programu mbalimbali ili kuwezesha sekta ya viwanda kuendeleza Biashara Ndogo na za Kati na kuongeza mchango wake katika ukuaji wa uchumi.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Maeneo ya kipaumbele katika kuendeleza Biashara Ndogo na za Kati kwa mwaka 2008/09 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuboresha sheria na taratibu za uanzishwaji na ukuzaji wa biashara;
- ii. Kuboresha fursa za upatikanaji mitaji kwa Biashara Ndogo na za Kati;
- iii. Kuimarisha ujasiriamali kwa kuwapa ujuzi na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kuendeleza sekta katika nyanja za teknolojia, masoko na taarifa sahihi; na
- iv. Kuimarisha mfumo wa taasisi wa kuendeleza sekta ya Biashara Ndogo na za Kati.

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i. Kuimarisha uwezo wa SIDO katika kuhudumia Biashara Ndogo na za Kati;
- ii. Kuendelea kutekeleza Mikakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA);

- iii. Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA);
- iv. Kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Kuendeleza Sekta Binafsi;
- v. Kusimamia utekelezaji wa Programu za Sera ya Biashara Ndogo na za Kati;
- vi. Kuandaa na kutekeleza Programu kwa ajili ya Biashara Ndogo na za Kati zilizopo Vijijini;
- vii. Kuandaa taratibu bora za upatikanaji wa maeneo ya kufanyia biashara, kuimarisha ajira kwa vijana, wanawake na walemavu; na
- viii. Kuimarisha matumizi ya viwango katika masoko kwa lengo la kuimarisha ushindani.

3.3.12 Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

a) Utangulizi

Serikali kwa kupitia MKURABITA inalenga kuhakikisha kuwa biashara na rasilimali za wananchi zilizo kwenye sekta isiyo rasmi zinarasimishwa ili ziweze kutambulika kisheria na hivyo kuwasaidia wamiliki kuzitumia rasilimali hizo kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Katika mwaka 2008/09, maeneo yatakayoendelea kushughulikiwa ni pamoja na:-

- i. Kuandaa utaratibu wa kasi zaidi (Fast tracking) wa kurasimisha ardhi za vijiji na kutoa hati miliki;
- ii. Kuandaa utaratibu wa kasi zaidi wa kurasimisha ardhi za mijini kwa mikoa miwili ya Tanzania Bara;
- iii. Kukamilisha upembuzi yakinifu juu ya uanzishwaji wa Masijala ya Kitaifa ya Masuala ya Biashara na Ardhi;

- iv. Kupanua wigo wa majaribio ya matumizi ya rasilimali katika kupata mikopo (mortgage finance) katika jiji la Arusha, Mbeya, na Zanzibar;
- v. Kukuza na kusimamia mahusiano ya kibiashara kati ya benki/vyombo vya fedha na wamiliki rasilimali na biashara;
- vi. Kutafiti uanzishwaji wa mifumo mipya ya usajili wa biashara ili kuimarisha utawala bora katika shughuli za biashara; na

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i. Kuandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi;
- ii. Kujenga masijala za vijiji na maabara za GIS za wilaya;
- iii. Kupima mashamba na kutoa hati miliki za kimila;
- iv. Kuendelea kuwahamasisha Watanzania kutumia rasilimali zilizorasimishwa kama dhamana kwa ajili ya kujipatia mikopo kutoka katika taasisi za fedha;
- v. Kuandaa utaratibu rahisi, wenye gharama nafuu, shirikishi na endelevu wa urasimishaji ardhi Vijijini na Mijini kwa mujibu wa sheria;
- vi. Kuandaa mfumo wa mawasiliano ya masijala hasa zinazohusu ardhi, watu (raia) na biashara kuanzia ngazi ya Kijiji/Shehia hadi Taifa ili kuweza kukusanya, kuhifadhi na kutoa taarifa sahihi kuhusu umilikaji mali na uendeshaji wa biashara;
- vii. Kurahisisha kanuni za kuanzisha, kuendesha na kufunga biashara;
- viii. Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Mawasiliano na wadau wa MKURABITA; na
- ix. Kukamilisha mwongozo wa kurasimisha rasilimali na biashara kwa mujibu wa sheria.

- x. Kuandaa warsha, semina na kutumia vyombo mbalimbali vya mawasiliano ili kutangaza matokeo ya tafiti zitakazofanyika na maboresho yatakatayopendekezwa; na
- xi. Kutoa mafunzo ya namna ya kutengeneza michanganuo ya biashara na kutunza mahesabu kwa wajasiriamali.

3.3.13 Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania 2020

a) Utangulizi

Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania (Tanzania Mini – Tiger Plan 2020) unalenga kuongeza kasi ya ukuaji uchumi na hatimaye kupanua ajira kwa Watanzania na hivyo kupunguza tatizo la umaskini wa kipato.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2008/09 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kukamilisha Ujenzi wa eneo maalumu la Uwekezaji la Benjamin William Mkapa na kuweka samani katika majengo ya kantini, kliniki, maduka pamoja na kituo cha zimamoto;
- ii. Kuanzisha Ujenzi wa kituo cha uwekezaji katika masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT-SEZ);
- iii. Kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya uanzishwaji wa maeneo maalumu ya uwekezaji katika mikoa ya Tanga, Kigoma na Pwani; na
- iv. Kuendelea kulitangaza Eneo Maalum la Uwekezaji la Mabibo ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i. Kukamilisha ujenzi wa kituo maalumu cha Uwekezaji cha Benjamin William Mkaia na kuweka samani Katika majengo ya kantini, kliniki, maduka, na kituo cha zimamoto na kuweka miundombinu ya majitaka pamoja na kufidia wakazi walio jirani ili kupisha ujenzi wa barabara ya kuzunguka eneo;
- ii. Kuanza ujenzi wa kituo cha uwekezaji katika masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT-SEZ);
- iii. Kuimarisha muundo mpya wa Mamlaka ya kusimamia maeneo maalumu ya uwekezaji; na
- iv. Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ujenzi wa maeneo maalumu ya uwekezaji katika mikoa ya Tanga ,Kigoma na Pwani.

Eneo la Pili: Uboreshaji wa Hali ya Maisha na Maendeleo ya Jamii

3.3.14. Sekta ya Elimu

a) Utangulizi

Serikali itaendelea na juhudi za uboreshaji wa sekta ya elimu katika ngazi zote. Aidha serikali itaendelea kushirikisha wananchi pamoja na sekta binafsi katika kutekeleza mipango ya kuinua kiwango cha elimu nchini.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Katika mwaka 2008/09 Serikali itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

- i. Kuongeza ujuzi na idadi ya walimu na wakufunzi kwa kutoa mafunzo zaidi kwa walio kwenye ajira na kuajiri wapya ili kuboresha uwiano wa mwalimu na wanafunzi katika ngazi zote;
- ii. Kujenga nyumba za walimu hususan kwenye maeneo yaliyo katika mazingira yasiyofikika kwa urahisi pamoja na ujenzi na

- ukarabati wa madarasa na nyumba za walimu katika maeneo ya shule;
- iii. Kujenga vituo vya elimu ya ufundi stadi katika wilaya nchini, kwa lengo la kuwa na kituo kila wilaya;
 - iv. Kujenga/kukarabati miundombinu muhimu ya kujifunzia kama vile madarasa, maktaba, maabara, kumbi za mihadhara na nyenzo za michezo;
 - v. Kutoa mafunzo ya elimu husishi na ya mara kwa mara ya ualimu kazini hasa katika masomo ya hisabati, sayansi na lugha ya Kiingereza na pia kusaidia kujenga utamaduni wa kupenda kujisomea kwa walimu, wanafunzi, na hata watu wengine;
 - vi. Kutoa mafunzo ya elimu ya ualimu tarajali na ualimu kazini ili kuinua taaluma na ujuzi wa walimu wanaofundisha katika shule na vyuo;
 - vii. Kuongeza kiwango cha udahili katika vyuo vya elimu ya juu na ya kati; na
 - viii. Kujenga vyumba vya mihadhara pamoja na nyumba za makazi ya wanafunzi katika vyuo vinavyotoa elimu ya juu.

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i. Kuhakikisha kuwa rasilimali fedha zinapatikana kwa wakati mashuleni na asasi nyingine za elimu;
- ii. Kuhakikisha kuwa mfumo wa taarifa za kimenejimenti za sekta ya elimu (ESMIS) unakamilika, unatekelezwa na kujengewa uwezo;
- iii. Kuliimarisha Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania;
- iv. Kuhakikisha kuwa upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, vya kimaandishi na visivyo vya kimaandishi, kwa wanafunzi wenye ulemavu na wasio na ulemavu unaboreshwa pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika ngazi zote;

- v. Kuimarisha programu ya elimu ya msingi nje ya mfumo rasmi wa shule;
- vi. Kuimarisha uongozi na uendeshaji wa elimu na mafunzo kwa kutoa mafunzo kwa watendaji;
- vii. Kuendelea kuimarisha na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Elimu za Msingi na Sekondari; na
- viii. Kuimarisha shughuli za ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi na utoaji wa ripoti za utekelezaji.

3.3.15 Sekta ya Afya

a) Utangulizi

Serikali itaendelea kutekeleza mipango mbalimbali ya kuimarisha sekta ya afya nchini. Katika mwaka 2008/09, pamoja na mambo mengine, juhudi zitaelekezwa katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2008/09 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuendelea na juhudi za kupunguza vifo vya watoto wachanga;
- ii. Kuendelea na jitihada za kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano;
- iii. Kupunguza vifo vya akina mama wakati wa ujauzito na kujifungua;
- iv. Kuboresha huduma za madawa ya kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI, huduma za kinga na kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;
- v. Kuhakikisha huduma za afya na ustawi wa jamii zinatolewa kwa kuzingatia masuala ya jinsia na uwiano wa kijiografia;
- vi. Kuboresha huduma za tiba ya Kifua Kikuu; na
- vii. Kuboresha na kuimarisha utafiti, mafunzo na maendeleo ya wataalam wa afya.

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa na vitendanishi muhimu kwa wakati uliopangwa katika ngazi zote;
- ii. Kuendelea kutoa huduma za kinga na tiba katika ngazi zote;
- iii. Kuboresha huduma za chanjo;
- iv. Kuongeza vituo vya kutolea huduma za mama na mtoto na vifaa kupitia Mkakati Kabambe wa Kupunguza Vifo vya Mama na Mtoto;
- v. Kuendelea kuzuia kuenea, kudhibiti na kutibu ugonjwa wa Kifua Kikuu na magonjwa nyemelezi kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI;
- vi. Kuongeza idadi ya vituo vya afya vijijini na mijini na kuboresha utoaji wa huduma hizo kwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM);
- vii. Kuendelea kukarabati na kupanua Vyuo vya Mafunzo ili kukidhi mahitaji ya rasilimali watu katika ngazi zote;
- viii. Kuimarisha na kuboresha huduma katika hospitali ya taifa;
- ix. Kuimarisha hospitali Teule za wilaya na za Mashirika ya Dini;
- x. Kuboresha huduma za ustawi wa jamii kwa makundi maalum katika jamii; na
- xi. Kuendelea kuhakikisha upatikanaji endelevu wa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI na kutoa elimu kuhusu matumizi ya dawa hizo.

3.3.16. Maji Safi na Maji Taka

a) Utangulizi

Serikali katika kipindi cha muda wa kati, 2008/09 -2010/11 inatilia mkazo zaidi katika kupanua na kukarabati miundombinu ya maji pamoja na kukamilisha miradi mbalimbali ya maji. Aidha, masuala ya kutunza mazingira na kushirikisha jamii katika nyanja zote za maendeleo ya maji mijini na vijijini yatapewa kipaumbele.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Katika mwaka 2008/09, maeneo ya kipaumbele yatakayotekelezwa ni pamoja na:-

- i. Kuendelea kupanua na kukarabati miundombinu ya usambazaji wa maji katika ngazi za mikoa na wilaya ili kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya mijini na vijijini;
- ii. Kuendelea kuchimba visima na mabwawa hasa katika wilaya zenye ukame;
- iii. Kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji ili kuvilinda vyanzo hivyo dhidi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira;
- iv. Kuimarisha uwezo wa utoaji wa huduma za maji safi na maji taka katika ngazi zote;
- v. Kuboresha miundombinu ya maji taka katika ngazi zote; na
- vi. Kupanua huduma ya upatikanaji wa maji kutoka Mradi wa Maji wa Ziwa Viktoria–Shinyanga–Kahama na kuueneza hadi kwenye vijiji vilivyopo kandokando ya bomba kuu la maji katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga.

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i. Kutoa miongozo ya utekelezaji na Usimamizi wa Maendeleo ya Mabonde ya Maji na usambazaji wa huduma za maji kibiashara kwa mawakala na mamlaka za maji mijini;
- ii. Kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji ili kuvilinda dhidi ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira;
- iii. Kusambaza taarifa muhimu kwa bodi za maji na wadau mbalimbali wa sekta ya maji;
- iv. Kukusanya na kuchambua sampuli za maji kutoka kwenye vyanzo vikuu vya maji na kusambaza matokeo ya uchunguzi wa sampuli hizo kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za tahadhari;
- v. Kusaidia kufanikisha shughuli za uchimbaji na ujenzi wa malambo na mabwawa;

- vi. Kuchimba visima vifupi na virefu katika maeneo mbalimbali; na
- vii. Kukarabati na kujenga miundombinu mbalimbali ya miradi mikubwa ya maji.

Eneo la Tatu: Utawala Bora na Uwajibikaji

3.3.17 Utawala bora

a) Utangulizi

Serikali inaendelea na jukumu la kulinda amani na usalama wa raia wake, pamoja na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji ili kutekeleza azma ya kuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa utawala bora na uwajibikaji, Serikali inawajibika kutumia rasilimali zake ili kuleta ulinzi na amani, kupiga vita rushwa na kudumisha utawala wa sheria.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Katika mwaka 2008/09, maeneo ya kipaumbele ni kama ifuatavyo:-

- i. Kuendelea kufuatilia uboreshaji na uimarishaji wa matumizi ya sheria zinazohusu kuzuia na kupambana na rushwa pamoja na zinazoimarisha uwazi, uwajibikaji na utawala bora;
- ii. Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya rushwa na jinsi wanavyoweza kushiriki katika vita dhidi ya rushwa;
- iii. Kuimarisha taasisi zinazosimamia Utawala Bora nchini;
- iv. Kuendelea, kuhimiza uwazi na uwajibikaji katika utendaji kwa ngazi zote;
- v. Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi, Asasi za Kiraia, Asasi Zisizo za Kiserikali na vyombo vya habari katika mapambano ya Serikali dhidi ya rushwa; na
- vi. Kuendelea kuratibu Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa na kuandaa taarifa za utekelezaji kwa kila robo mwaka.

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i. Kuboresha uwezo wa watendaji na vyombo vya kulinda sheria;
- ii. Kujenga mazingira mazuri/bora ya watumishi wa umma katika sekta ya sheria;
- iii. Kutoa nyenzo na miundombinu ya kufanya kazi;
- iv. Kuhakikisha usalama wa raia na utoaji haki ya kisheria kwa muda muafaka;
- v. Kuboresha mawasiliano kati ya Serikali na wadau wengine juu ya kupiga vita rushwa katika Utumishi wa umma.;
- vi. Kuwahusisha wadau wote katika kutekeleza awamu ya pili ya Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa;
- vii. Kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha umma juu ya madhara ya rushwa na njia za kuipiga vita; na
- viii. Kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za taifa kwa usawa, uwazi na uwajibikaji.

3.3.18 Vita Dhidi ya UKIMWI

a) Utangulizi

Serikali imeendelea kulipa umuhimu wa pekee suala la janga la VVU/UKIMWI kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Kutokana na juhudi za Serikali za kupambana na janga hilo hasa baada ya kampeni ya Mheshimiwa Rais juu ya kupima kwa hiari na kupokea ushauri nasaha, idadi ya watu wanaojitokeza kupima kwa hiari imeongezeka.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Katika mwaka 2008/09, maeneo ya kipaumbele yatakayotekelezwa ni pamoja na:-

- i. Kuongeza juhudi za kufanya watu wabadili tabia ili kupunguza kasi ya kuenea kwa maambukizi;
- ii. Kuimarisha huduma za majumbani kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI;

- iii. Kuendelea kuongeza idadi ya wale wanaonufaika na huduma ya kupatiwa madawa ya kupunguza makali ya UKIMWI;
- iv. Kuzuia ongezeko la maambukizi hasa kwa vijana na wale wote walio na uwezekano mkubwa zaidi wa kueneza maambukizi haya kama wanaofanya biashara ya ngono;
- v. Kuhakikisha kuwa shule za msingi na sekondari zinaendelea kuelimisha juu ya stadi za maisha kuhusiana na virusi vya UKIMWI na UKIMWI.

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i. Kuwasaidia kiuchumi na kijamii wale wanaoishi na VVU/UKIMWI;
- ii. Kuendelea kutungamanisha masuala ya UKIMWI kwenye mifumo ya kitaifa ya fedha na mipango;
- iii. Kuendelea kuhamasisha watu wa rika zote juu ya huduma na matibabu kwa walioambukizwa kwa kutumia taarifa za kiTOTAL za kijamii na elimu ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI;
- iv. Kuendelea kuimarisha huduma za nyumbani na matibabu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI;
- v. Kuhimiza matumizi ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI (ARVs);
- vi. Kufuatilia matumizi bora ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya UKIMWI; na
- vii. Kuzingatia vipaumbele vilivyotolewa kwenye mfumo wa Mpango Mkakati wa Kitaifa pamoja na Mpango Kazi wake.

3.3.19 Mazingira

a) Utangulizi

Serikali imeandaa Programu ya Taifa ya kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ili kukabiliana na matatizo ya mazingira na athari zake. Baadhi ya athari hizo ni pamoja na zile zinazotokana na

uharibifu wa vyanzo vya maji na ukanda wa ozoni, kuenea kwa hali ya jangwa na ukame, usafirishaji wa kemikali baina ya nchi na nchi, upotevu wa baioanuai na mmomonyoko wa ardhi.

b) Mpango wa Mwaka 2008/09

Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2008/09 ni kama ifuatavyo:-

- i. Kusimamia utekelezaji wa sera ya mazingira na mikakati yake na kukuza weledi juu ya uhusiano kati ya mazingira, umaskini na maendeleo endelevu;
- ii. Kutekeleza mikakati, programu na miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira; na
- iii. Kutekeleza mikataba na itifaki za kikanda na kimataifa zinazohusu hifadhi ya Mazingira.

c) Mikakati

Mwaka 2008/09 Serikali inalenga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- i. Kukamilisha maandalizi ya Muundo wa Utoaji wa Taarifa wa Mazingira;
